
SportPesa
TZS. 1,144,195,580
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



Utata manispaa kulipia mamilioni taa za barabarani

UKURASA 5




Nipashe
Jumamosi Aprili 16, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580917
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


## IJUMAA KUU

# Ujumbe haki, amani na upendo watawala

**MAASKOFU** wakemea uonevu, unyanyasaji, wataka watu wajifunze kusamehe, Ruwa'ichi akemea viongozi vigeugeu ... *Endelea Ukurasa. 2 & 3*



Kijana Andrea Clement, akiwambwa msalabani wakati wa igizo la mateso ya Yesu Kristo, katika ibada ya Ijumaa Kuu kwenye Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria Mpalizwa Mkwawa, mjini Iringa jana. Picha zaidi Uk. 18. **PICHA: FRANCIS GODWIN**



Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Suzanne Ndomba-Doran (wa pili kulia), akimpongeza Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Sabasaba Moshingi, baada ya benki hiyo, kuibuka mshindi wa jumla kwenye hafla ya chakula cha usiku ya NACTVET, kwa ajili ya kuwatambua na kuwatunuku waajiri vinara wa kukuza ujuzi na vipaji nchini, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. Kulia ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Eliamani Sedoyeka na Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), Dk. Adolf Rutayuga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mbunge alia na ukatili kiuchumi, adai chanzo cha matukio ya unajisi

UKURASA 4

## Kashfa Uhamiaji stika feki viwanja vya ndege

UKURASA 4

MICHEZO NYONI:TUMEJIPANGA KWA ORLANDO UK.23 | MAONI, KATUNI UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa katika mazungumzo na Rais wa National Democratic Institute (NDI), Dk. Derek Mitchell, jijini Washington DC, Marekani juzi. **PICHA: IKULU**

# Ujumbe amani, haki, upendo watawala ibada Ijumaa Kuu

**Na Waandishi Wetu**

UJUMBE wa amani, upendo, haki na kusamehe vilitawala jana katika ibada za makanisa mbalimbali nchini wakati wa ibada ya Ijumaa Kuu.

Wakristo nchini jana waliungana na wenzao duniani kote kuadhimisha kuteswa na kufa kwa Yesu Kristo yapata miaka 2,000 iliyopita.

Katika ibada za Ijumaa Kuu, maaskofu na wachungaji wa makanisa mbalimbali wakati wa mahubiri yao walisisitiza Watanzania kudumisha amani, upendo na kusamehe kama alivyofanya Yesu Kristo wakati akisulubiwa msalabani.

Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mbeya, Gelvas Nyaisonga amewataka wakristo wote nchini kukumbuka kuteswa na kufa kwa Yesu Kristo kwa kuacha kutenda maovu, akisisitiza kuwa ndilo lengo kuu la kumbukizi hiyo.

Nyaisonga ambaye ni Rais wa Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki (TEC), aliyasema hayo jana alipokuwa anahubiri kwenye Ibada ya Ijumaa Kuu iliyofanyika katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Antony wa Padua.

Pamoja na mambo mengine, Askofu Nyaisonga alisema damu ya Yesu iliyomwagika msalabani ilikuwa inaashiria utakaso.

**ASKOFU MALASUSA**

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa, alisema kifo cha Yesu hakitakuwa na maana yoyote kama watu watabaki katika minyoyoro ya utumwa katika kufanya mambo yasiyompendeza Mungu.

"Kifo cha Yesu hakitakuwa na maana tukibaki katika rangi ya nguo, tukibaki katika utamaduni wa kutokula kitu fulani na kula kitu fulani.

Kifo cha Yesu kitakuwa na maana pale tu tutakapoweka uhusiano wetu na Mungu sawa sawa.

"Wengine ndani ya familia tumeruhusu unyanyasaji, mateso kwa ajili ya watu wengi, roho ya Pilato bado ipo. Pilato alihangaika sana akafikiri kunawa kunamwondolea hatia.

Alipewa nafasi ya kusema 'huyu hana hatia' lakini sauti za watu na wengi tumeondoka katika msimamo wetu kwa sababu ya sauti za watu," alisema.

Dk. Malasusa Alisema wanaume wengi wamepewa nafasi lakini wameshindwa kusimamia lile Mungu anakusudia katika familia.

"Wazazi wengi tumeshindwa kusimamia watoto kwa kuogopa utachukiwa na watoto. Watu wenye nafasi mbalimbali ofisini wameshindwa kusimamia iliyo kweli kwa sababu wanapenda kupendwa.

Sote hata katika kanisa tumeshindwa kusimamia kweli, roho ya Pilato bado inakula ulimwengu," alisema.

Naye Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Arusha, Mhashamu Isaac Amani, alisema wakristo wanapoishi katika ukristo wao amani inatawala.

**TUACHE VISASI**

Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Shinyanga, Liberatus Sangu, amewataka Watanzania kuishi kwa kusameheana, ili kuepuka visasi ambavyo husababisha mafarakano.

Kwa upande wake, Askofu wa Umoja wa Makanisa ya Kikristo ya Pentekoste Tanzania (CPCT), Ayoub Muna, aliwataka waumini wa kikristo kubadilisha matendo yao na kuacha kujiingiza kwenye uhalifu na vitendo vinavyomchukiza Mungu.

Akihubiri jana kwenye ibada ya Ijumaa Kuu ya Umoja wa Kanisa Mkoa wa Arusha (UKAMA), Askofu Muna alisema Yesu Kristo anapokamatwa kwenye uhalifu ni aibu kwa Wakristo.

Alisema baadhi ya Wakristo utawatambua wakiwa hawana vyeo, lakini pale wanapopata vyeo inakuwa shida kwa wengine jambo ambalo siyo sahihi, hivyo ni vyema watu wakabadilika na kuishi katika ukristo wao.

**KUSAIDIA WENYE DHIKI**

Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Anglikana, Mtaa wa Madaba wilayani Muheza, Paul Luhinga, aliwaomba Watanzania kuendelea kuombea nchi kuwa na amani, viongozi kufanya matendo ya huruma ya kuwasaidia wenye dhiki na kutokata tamaa.

Alisema Ijumaa Kuu ni siku maalumu ya mwaka ambayo wafuasi wengi wa Yesu Kristo wanaadhimisha kifo chake msalabani.

Mchungaji Msaidizi Namba Tatu wa kanisa hilo, Ernest Shedawa, alisema waumini kipindi hiki wawe na moyo wa msamaha na kutolipiza ubaya kama ilivyokuwa kwa Yesu Kristo. Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Anglikana la Chumbageni Jijini Tanga, Kenan Aidan Kamote amesema wakati wanapoelekea Sikuuu ya Pasaka ni vyema Watanzania wakajenga tabia ya kusameheana kama wanadamu iwapo watu wamekoseana.

**KUMTANGULIZA MUNGU**

Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini, Usharika wa Mjini Kati Arusha Kati, Daniel Sadera, aliwataka wakristo wa kanisa hilo, kumtanguliza mbele Mungu hata wanapopita katika hali ngumu ya maisha.

Alitoa wito huo kwa wakristo wa kanisa hilo jana wakati wa ibada ya Ijumaa Kuu ya kumbukumbu ya kifo cha Yesu Kristo.

"Hata tunapopitia katika kipindi kigumu cha maisha kutokana na ugumu wa maisha tunatakiwa kumtanguliza Mungu mbele kwa kuwa yeye ataifanya njia kuwa nyepesi,"alisema.

**●Imeandaliwa na Na Cynthia Mwilolezi, Allan Isack (Arusha), Steven William (Muheza), Osca Assenga (Tanga), Marco Maduhu (SHINYANGA), Romana Mallya (Dar), Renatha Msungu, Paul Mabeja na Peter Mkwavila (Dodoma), Ashton Balaigwa (Morogoro) na Nebart Msokwa, (MBEYA)**

## Viongozi wapewa somo kutenda haki

**Na Epson Luhwago**

VIONGOZI na watu wenye mamlaka wametakiwa kutenda haki na kutoa uamuzi katika nafasi walizopewa bila kuogopa watu, kujali ukabila, udini na uzawa.

Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Morogoro, Lazarus Msimbe , alisema hayo jana wakati wa ibada ya kitaifa ya Ijumaa Kuu iliyofanyika katika Kanisa Kuu la Morogoro.

Ibada ya Ijumaa Kuu ilifanyika katika makanisa mbalimbali nchini kwa Wakristo nchini wakiungana na wenzao duniani kukumbuka kuteswa na kufa kwa Mwokozi wao, Yesu Kristo karibu miaka 2,000 iliyopita.

Kiongozi huyo alitoa mfano wa Pilato aliyekuwa na mamlaka wakati wa Yesu lakini kutokana na kuogopa Wayahudi, alishindwa kutoa haki na kumwachia akahukumiwe nje ya mfumo wa uongozi.

"Pilato anatufundisha mengi. Anaonyesha ni kiongozi wa namna gani kwani alijua Yesu Kristo hakuwa na hatia lakini aliogopa macho ya watu na kutoa uamuzi usio sahihi na haki. Hata sasa wako baadhi ya watu waliopewa mamlaka katika jamii kwenye nafasi mbalimbali lakini wanashindwa kutoa uamuzi sahihi na haki kwa sababu ya uoga.

"Tunapaswa kujifunza kupitia jambo hilo kwa kutenda haki katika nafasi zetu. Tusiwatenge watu kwa sababu ya udini, ukabila na uzawa. Usiseme siwezi kukupa kazi kwa sababu wewe si wa dini yangu, wewe si wa kabila langu au wewe si wa taifa langu.

"Tutende haki bila ubaguzi wowote. Tuthibitishe ukweli pia badala ya kupindisha ukweli kwa maslahi binafsi. Ubinafsi na kutotenda haki kumesababisha watu kupata shida, kunyanyaswa na kuteswa," alisema. Askofu Msimbe pia aliwakumbusha Wakristo kuwa kielelezo cha Yesu Kristo kuhusu upendo kwa watu wengine kwa kuwahurumia na kuwasaidia walio katika matatizo mbalimbali.

"Tuwajibike kwa ajili ya wengine kama Yesu alivyofanya. Waliokata tamaa watiwe moyo, walio dhaifu wasaidiwe, wapinzani wa injili waelekezwe, wajinga wafundishwe, wenye majivuno wafundishwe unyenyekevu, maskini wasaidiwe, wanaonyanyaswa wakombolewe, wema wapongezwe na wabaya waonywe," alisisitiza.

Askofu Msimbe pia aliwakumbusha Wakristo kwamba katika maisha yao watambue kwamba kuna kifo, hivyo wajiandae kwa maisha yajayo baada ya ukomo wa maisha ya duniani.

Alisema kwa kutambua kwamba kuna kufa kama ilivyokuwa kwa Yesu Kristo, wasiogope kufa bali wajiandae kwa maisha yajayo kwa kutenda mema.

"Lakini wako watu ambao wanaogopa kufa. Sababu kubwa ni tatu. kwanza, kwa sababu ya mali zao. Wanaogopa ni kuwaza mali zao watamwachia nani. Sababu ya pili ni ndugu, jamaa na marafiki hata familia kwamba wataachana nao vipi. Lakini jambo la tatu ni hukumu.

"Hili la tatu (hukumu) ndilo ambalo linawasumbua wengi. Lakini naomba niwaambie kuwa hukumu hiyo isiwape hofu bali watu watende mema kwa ajili ya kuepuka hiyo hukumu," alisema.



Sheikh Mkuu wa Tanzania, Mufti Abubakar bin Zuberi Ally (katikati) na Ofisa Mkuu wa wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (kulia), wakiwa katika futari iliyoandaliwa na benki hiyo, kwa ajili ya wateja wake, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ruwa'ichi akemea wasio na msimamo

**Na Mwandishi Wetu**

ASKOFU Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Yuda Thadei Ruwa'ichi, amekemea tabia ya baadhi ya watu wakiwamo viongozi kutokuwa na msimamo na kuendekeza unafiki na kuwa vigeugeu.

Katika mahubiri yake ya Ibada ya Ujumaa Kuu jana katika kanisa la mtakatifu Kilbe, Parokoa ya Mwenge, Dar es Salaam, Askofu Mkuu Ruwa'ichi alisema baadhi ya watu wanajionyesha kuwa ni watu wa Mungu lakini matendo yao ni kinyume cha ushuhuda wa Yesu Kristo. Alisema katika maisha ya sasa, wako watu katika jamii wanamchekea mtu usoni lakini moyoni wako tofauti kabisa kutokana na kutokuwa na msimamo juu ya wayasemayo hawatendi haki.

"Wakati Yesu anaingia Yerusalemu, watu walimpokea kwa shangwe lakini hao hao walikengeuka na kusema asulubiwe. Hata sasa kuna watu wanajibainisha kama watu wa Mungu lakini ni watu wasio na msimamo, wasio waadilifu na wasio watenda haki," alisema.

Kutokana na kuwapo kwa watu wa namna hiyo, aliwataka Wakristo kukumbuka mateso na kufa kwa Yesu Kristo kwa kutenda mema na kuwajali watu pamoja na kujishusha na kuwa wanyenyekevu.

Askofu Ruwa'ichi alisema iwapo jamii itakuwa na watu watenda mema, waadilifu na wenye kujali maisha ya watu wengine, jamii na taifa litakuwa na amani na hakutakuwa na watu wanaonyanyaswa wala kunyimwa haki.

Alisema hata baadhi ya watu waliopewa nyadhifa katika nafasi mbalimbali, wamekuwa na tabia kama ya Pilato (aliyekuwa mtawala wakati Yesu Kristo anasulubiwa) ambao wamekuwa wakishindwa kutenda haki na kutumia nafasi zao kwa maslahi binafsi.

"Siku hii ya leo (Ijumaa Kuu), tunajifunza habari za Pilato ambaye alishindwa kutenda haki kutokana na nafasi yake. Hata sasa katika jamii, tunao viongozi ambao hawathubutu kusimamia haki, ukweli na kuwatetea wanyonge.

"Sasa ni wakati wa kutafakari kuteswa na kufa kwa Yesu Kristo kwa kutafakari maisha yetu, tujipime vizuri na kusimamia haki, ukweli na kuwa watetezi wa wanyonge. Hiyo ndiyo tabia ya Yesu Kristo na ndio upendo aliouonyesha kwetu sisi wanadamu," alisema.

# Wazazi wapewa somo malezi na ustawi familia

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAZAZI wametakiwa kudumisha upendo furaha na amani huku wakitanguliza msamaha kwa kila jambo linalotokea miongoni mwa wanafamilia.

Hayo yalisemwa jana katika ibada ya Ijumaa Kuu iliyofanyika katika Parokia ya Kristo Mfalme Jimbo la Moshi iliyoongozwa na mwakilishi wa Askofu Ludovick Minde, Padri Josephat Swai.

Alisema wazazi na walezi wanapaswa kuhimiza amani na upendo katika familia kwa kuwa ngazi hiyo ndiyo chimbuko la jamii na taifa kwa ujumla.

"Wazazi ni chemchemi ya kuwaelekeza watoto kuishi tunu za imani (furaha, amani na upendo). Tufanye kazi za kuyasimamia haya ili watoto wetu wayafanye hivyo na kuepusha migogoro katika jamii," alisema.

Akiwa katika maandamano ya njia ya msalaba, Askofu Minde aliwataka waamini wa jimbo la Moshi kufanya maombi maalumu kwa ajili ya kuombea nchi zinazomwaga damu.

"Tutumie siku ya leo (Ijumaa Kuu) katika kuhakikisha tunafanya maombi maalumu kwa ajili ya nchi zinazomwaga damu za watu kwa ajili ya vita," alisema.

Adha, aliwataka vijana kuwa na jitihada za kumtafuta Mungu na kuacha tabia za kutafuta fedha za haraka.

"Tutafute kwanza ufalme wa Mungu. Tujitahidi kutenda mema, tuache fikra za kuwaumiza wenzetu kwa ajili ya kupata mali za haraka. Kadhalika, wazazi acheni kuwa sababu ya ugonvi na chanzo cha migogoro hasa kwa watoto wenu kwenye ndoa zao," alisema Askofu Minde.

Baadhi ya washiriki wa ibada hiyo, akiwemo Laurence Mshio, waliomba kanisa kuendeleza amani na kuongeza upendo kwa familia.

# Maaskofu wataka waumini kuacha visasi

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisani Katoliki Jimbo Kuu la Dodoma, Beatus Kinyaiya, amewataka waumini kujifunza kusamehe badala ya kuchukua uamuzi wa kujitoa au kutoa uhai wanapokosewa.

Akihubiri katika ibada ya Ijumaa Kuu, Kanisa Kuu la Mtakatifu Paulo wa Msalaba jana, Askofu Mkuu Kinyaiya alisema kukaa na msongo wa mawazo moyoni kunachangia watu kujitoa uhai kwa kujiua, kujinyonga na kusababisha taifa kuwa na vifo vingi.

Kinyaiya alisema vifo vingi vinatokea kwenye ndoa, hospitalini na wengine hujinyonga kutokana na watu kushindwa kusamehe na kukaa na vitu moyoni.

"Tujifunze kusamehe kama alivyofanya Yesu Kristo msalabani. Tukifanya hivyo itachangia kupunguza vifo hapa nchini," alisema.

Pia aliikumbusha jamii kupenda kufanya toba kwa ajili ya kujiweka sawa kiimani jambo litakalofanya kupunguza msongo wa mawazo ambao huchangia mtu kufanya mambo mabaya pale anapoona ameelemewa.

**ASKOFU ATAKA KUSAMEHE**

Naye Askofu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Dayosisi ya Central Tanganyika, Dk. Dickson Chilongani, amewataka viongozi wa kisiasa kujenga tabia ya kusameheana bila kuwapo kwa masharti na kuacha kulipiza visasi.

Akihubiri ibada ya Ijumaa Kuu katika Kanisa Kuu Anglikana la Roho Mtakatifu jana jijini hapa, alisema viongozi wanapaswa kuacha kulipiza visasi kwa kuwa hali hiyo inachangia taifa kugawanyika.

"Ni lazima kujenga tabia ya kusamehe kama ambavyo Yesu Kristo anatukumbusha katika mateso yake na tunapaswa kuacha kulipizana visasi kwani Mungu anatutaka tusichoke kusamehe. Nasema samehe saba mara sabini," alisema Askofu Dk. Chilongani.

Pia aliwataka wanasiasa nchini kujenga umoja mshikamano kwa kumaliza tofauti zao kwa kukaa meza moja ya majadiliano.

Kadhalika, alisema ugumu wa maisha unaolalamikiwa hivi sasa na wananchi unatokana na watendaji wa serikali kutowajibika katika nafasi zao na vita vya Russia na Ukraine sio sababu ya msingi.

"Yapo mambo mengi ambayo yanasababisha ugumu huu wa maisha ambao unalalamikiwa na Watanzania ikiwemo viongozi wa serikali kutowajibika. Tumeona hivi sasa nidhamu ya kazi imeshuka, matumizi ya fedha yamebadilika, lakini pia rushwa hivi sasa imerudi. Tunaona matrafiki njiani wanaomba rushwa.

"Rais anapenda kuendeleza yale ya awamu ya tano lakini viongozi wake huku chini wao wamejisahau sana kana kwamba awamu ya tano iliondoka na kila kitu sifikirii kama vita ndiyo sababu kuu ya kupanda kwa maisha nchini,"alisema.

Vilevile, alisema sababu nyingine ni ukame ambao umechangia ugumu wa maisha na kuishauri serikali kufunga mipaka ambayo inatumika kusafirisha na kuuza chakula nje.

**Imeandaliwa na; Renatha Msungu, Paul Mabeja na Peter Mkwavila.**

# Mbunge alia na ukatili wa kiuchumi

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Iringa Mjini, Jesca Msambatavangu (CCM), amesema wanaume wengi hawana uwezo wa kumudu kugharamia mapenzi, hali inayowafanya wakimbilie kwa watoto wasio na hatia na kuwafanyia ukatili wa kingono.

Amesema hilo linatokana na alichokiita ukatili wa kiuchumi unaowakabili wananchi wengi kwa sasa nchini, akiinyoshea kidole serikali kwa kushindwa kuwa na mikakati mizuri ya kuwainua wananchi wake kiuchumi.

Jesca alitoa kauli hiyo bungeni juzi alipochangia hoja ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI ) kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Mbunge huyo alipinga hoja ya Mbunge wa Viti Maalum, Esther Matiko (CHADEMA) kwamba mwanaume anayethibitika kufanya ukatili wa kingono ahasiwe, akisema zipo sababu zinazosababisha wanaume kuwanajisi watoto wadogo, zikiwamo ukata na ushirikina.

"Mapenzi ni product (bidhaa) kama products zingine, vijana hawana nguvu ya kununua wanakwenda kwa watoto wadogo na kuwaonea. Kwa nini wamepunguza nguvu ya kununua mapenzi? Ni kwa sababu ya ukatili wa kiuchumi ikiwamo na sisi hapa tunachangia," alisema.

Jesca alifafanua kuwa kama kuna wizara ambayo haiwezi kutoa kipaumbele kwa Watanzania katika miradi inayotekelezwa na serikali, hiyo ndiyo inasababisha matatizo hayo ya ukata na ukatili wa kijinsia.

Bila kutaja aliyesema, Jesca alisema "Mtu anaposema nguzo zote zinunuliwe nje ya nchi, vijana walioanda miti katika mikoa mbalimbali watapata wapi fedha za kununua mapenzi watakapokuwa na hitaji la mapenzi?

"Sasa hivi hakuna mwanamke atakupenda sura, hakuna mwanaume mwenye sura nzuri, unampendaje mwanaume sura? Mwanaume anapendwa kitu alichonacho, anapendwa kwa pochi.

"Wanaume rijali wataenda wapi na ana hamu ya kufanya mapenzi? Mnakwenda kuwabana machinga badala ya kuwajengea mazingira mazuri ya kufanya kazi wawe na uwezo wa kununua penzi."

**DUA KUKEMEA 'JUJU'**

Huku akiibua shangwe bungeni, Jesca aliendelea na hoja yake, akisema kama ushirikina unachangia vitendo vya ukatili wa kingono nchini, inashughulikiwa kiroho kwa kutumia nguvu za Mungu.

Jesca aliwataka wabunge wanaoamini kufuatana naye katika dua fupi aliyoitoa bungeni wakati akichangia.

"Mungu tusaidie, hatutawahasi kama alivyosema mheshimiwa (Esther Matiko) lakini tuachilie nguvu za Mungu kuanzia hapa zikawashughulikie wote.

"Katika kile kiungo wanachotumia kulawiti watoto wetu, kipigwe nguvu kisifanye kazi na zile mashine mbili zinazozalisha nguvu zipotee kabisa na daktari utakapoona dalili hizo anitafute. Arudi katika hali ya kawaida tumfanyie ushauri nasaha ili watoto wetu wawe salama," alisema.

**WANAUME WANAOPIGWA**

Awali, Jesca alirejea takwimu zilizotolewa na serikali zinazoonyesha asilimia 33 wanaofanyiwa ukatili ni watoto na asilimia 67 ni wanawake.

Hata hivyo, mbunge huyo alisema upo pia ukatili dhidi ya wanaume na utafiti unaonyesha kuwa kiwango cha wanaume kupigwa na wake zao kimeongezeka hadi asilimia 71.7 wakati wanawake waliopigwa ni asilimia 73.5.

"Na kwa kiwango hicho wanaume wanashuka kwa kupiga na wanawake wanapanda kwa kasi kubwa," Jesca alisema na 'kulipua' Bunge kwa vicheko.

Alisema kwa hali inavyoendelea inaonekana kuwa athari zinawaangukia watoto kwa kuwa vipigo vinapoendelea ndani ya nyumba, ustahimilivu unakuwa haupo na kusababisha ndoa kuvunjika, hivyo kuweka mazingira hatarishi kwa watoto.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akikabidhi Tuzo ya Amani kwa Mshauri wa Kamati ya Amani, Altaf Hirani, baada ya kushiriki futari iliyoandaliwa na kamati hiyo, jijini Dar es Salaam, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kashfa Uhamiaji stika feki viwanja vya ndege

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebaini hasara ya mabilioni ya shilingi kutokana na matumizi ya stika za viza za kughushi yaliyofanywa na Idara ya Uhamiaji (sasa Jeshi la Uhamiaji) kwa wageni walioingia nchini kupitia viwanja wa ndege.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Jumanne, CAG Charles Kichere anasema alibaini hali hiyo baada ya kufanya ukaguzi wa kiuchunguzi wa mapato ya viza yaliyokusanywa na Idara ya Uhamiaji kutoka kwa wageni walioingia nchini kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

Anafafanua kuwa Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 (iliyorejewa mwaka 2016) inaipa mamlaka Idara ya Uhamiaji kukusanya na kusimamia mapato yatokanayo na viza, pasi na vibali.

CAG anabainisha kuwa Agosti 2, 2019, Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI) alibaini kuwapo kwa stika za viza za kughushi katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA).

Anabainisha kuwa uchunguzi wa awali uliofanywa na DCI, ulibaini kuwa stika za viza za kughushi ziliuzwa na Idara ya Uhamiaji kwa wageni walioingia nchini kupitia (KIA).

"Kufuatia hali hiyo, DCI aliiomba ofisi yangu ifanye ukaguzi wa kiuchunguzi. Ukaguzi huu ulilenga kubaini hasara ambayo serikali imepata na kuwabaini maofisa wa Uhamiaji waliohusika katika kashfa hiyo kuanzia kipindi cha tarehe 01 Januari 2019 hadi 30 Juni 2019. "Katika uchunguzi huo, ilibainika serikali imepata hasara ya Sh. bilioni 2.42 kutokana na stika 21,208 za viza zinazodaiwa kughushiwa na ambazo kumbukumbu zake zilifutwa kwa makusudi kwenye Mfumo wa Maombi ya Viza (VAS) na maofisa Uhamiaji wa KIA.

"Kabla ya tarehe 23 Agosti 2019, Idara ya Uhamiaji ya KIA ilikuwa inatumia Mfumo wa Maombi ya Viza (VAS) kurekodi maelezo ya wageni wanaolipia viza wakati wa kuwasili pamoja na wale wenye viza zisizolipiwa (gratis VISA). "Kiutendaji, kurekodi katika VAS kulikamilishwa baada ya mgeni husika kulipa ada za viza na kupokea stakabadhi ya mapokezi ya fedha za serikali (ERV).

"Hakukuwa na kumbukumbu zilizowekwa katika VAS zinazohusu wanadiplomasia, vibali vya wakazi, vyeti vya misamaha, pasi, wakazi wanaorejea, viza za mtandaoni na viza zilizotolewa kwenye balozi," anafafanua.

Pamoja na kuwapo kwa VAS, CAG pia anasema kulikuwa na mfumo wa PISCES ambao ulikuwa unafuatilia masuala yote ya kiusalama.

Ili kuhakikisha kuwa hakuna Mtanzania au mgeni ambaye amepigwa marufuku, ama aliyewekewa vikwazo kuingia katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, CAG anasema ilikuwa ni lazima abiria wote waliotua kupitia KIA wapitie kwenye mfumo wa PISCES.

Hata hivyo, CAF anasema kuanzia Januari Mosi, 2019 hadi Juni 30, 2019, ukaguzi wake ulibaini kuwa Watanzania 41 na wageni 107,119 waliwasili nchini kupitia KIA.

Kati ya wageni 107,119 waliowasili nchini kupitia KIA, wageni 11,341 walipata viza kwa njia ya mtandao, wageni 7,044 walipata viza kutoka kwenye ofisi za balozi zilizoko katika nchi mbalimbali.

CAG anafafanua kuwa wageni 13,678 hawakuwa na viza kutokana na sababu mbalimbali, zikiwamo misamaha, pasi, mikataba na zinginezo, na wageni 41,286 walilipa viza walipowasili nchini kupitia KIA.

"Ukaguzi pia ulibaini wageni 212 walipata na kulipia viza kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume lakini walitua KIA.

"Wageni 33,558 waliwasili kupitia KIA ingawa taarifa zao ambazo ni pamoja na stakabadhi za mapokezi ya fedha (ERV), fomu za kuingia nchini pamoja na taarifa za uwekaji fedha benki hazikupatikana.

"Kwa sababu hiyo, sikuweza kujua ni kiasi gani cha mapato ambayo serikali ilipaswa kupata kutoka kwa wageni hao. Katika uchunguzi zaidi, niligundua kuwa taarifa za stika 21,208 za viza za wageni waliowasili nchini kupitia KIA zilifutwa kabisa kutoka kwenye kanzidata ya mfumo wa VAS.

"Stika hizo zilizoondolewa ziliwahusu wageni ambao walipaswa kulipa viza walipowasili, lakini maofisa 32 wa Idara ya Uhamiaji KIA wamedaiwa kufanya njama na kuwapatia wageni hao stika za viza za kughushi na kujipatia Sh. bilioni 2.42 kutoka kwao.

"Katika kubaini jinsi udanganyifu huo ulivyopangwa na kufanyika, ukaguzi ulibaini kuwa udanganyifu huo ulifanyika kutokana na dosari katika mfumo wa VAS ambao ulionekana kwa urahisi.

"Kufuatia uchunguzi katika mfumo wa VAS, ilibainika kuwa mfumo huo unaruhusu taarifa za stika za viza kuchapishwa kabla ya kuhifadhiwa na kwamba maelezo ambayo hayajahifadhiwa yanaweza kufutwa bila ya kuwapo na idhini.

"Zaidi ya hayo, mfumo wa VAS pia unaruhusu maingizo yaliyofutwa kuondolewa kabisa kutoka kwenye kanzidata bila ya hitaji la hatua zozote za urejeshwaji kutekelezwa," anasema.

CAG anaendelea kubainisha kuwa kutokana na upungufu wa mfumo wa VAS, ukaguzi ulithibitisha kuwa maofisa 32 wa Idara ya Uhamiaji KIA walipokea fedha kutoka kwa wageni na walichapisha taarifa zao kwenye stika za viza za kughushi bila kuhifadhi kwenye mfumo wa VAS na kufuta taarifa zao kwenye kanzidata ya mfumo wa VAS.

Anasema kuwa katika maingizo ya taarifa 21,208 ya stika za viza zilizoondolewa kwenye mfumo wa VAS, serikali ilipata hasara ya Sh. bilioni 2.42 kwa kipindi cha miezi sita, kuanzia Januari Mosi, 2019 hadi Juni 30, 2019.

"Ninapendekeza Idara ya Uhamiaji ichukue hatua stahiki za kisheria na kinidhamu dhidi ya maofisa 32 wa Idara ya Uhamiaji wa Kituo cha KIA ambao wanahusika kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 2.42," CAG anatoa hoja.

# DAWASA yawataka wakazi kuomba maji

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa Kata ya Mbwawa katika Mji wa Mlandizi, Kibaha mkoani Pwani, wamehamasishwa kujitokeza kwa wingi kuomba huduma ya maji kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) baada ya kukamilika kwa mradi wa maji wenye thamani ya Sh. bilioni 1.1.

Meneja wa DAWASA Mlandizi, Mhandisi Damson Mponjoli, alisema hayo jana wakati wa kikao cha uhamasishaji wananchi hao kujitokeza ili kunufaika na huduma ya majisafi.

"DAWASA tumetekeleza mradi mkubwa wa Maji ambako fedha nyingi za Serikali takribani shilingi bilioni 1.1 zimetumika kwenye mradi huu ambao nanyi ni wanufaika, hivyo niwaombe mjitokeze kwa wingi kuomba huduma hii ili azma ya kumtua mama ndoo ya maji kichwani ifikie" alisema.

Aliwahakikishia wananchi kuwa DAWASA imejipanga kuwahudumia na kwa kuanza inatenga siku ya Jumamosi kupita nyumba hadi nyumba kufanya zoezi la kuwatambua wananchi wanaohitaji huduma ya majisafi katika kata hiyo.

Ofisa Mawasiliano DAWASA, Elizabeth Eusebius, aliwaeleza wakazi wa Mbwawa umuhimu wa kujiunga na huduma ya majisafi kutoka DAWASA ambayo ni salama kwa afya na yenye unafuu wa gharama.

"Gharama za maji ya DAWASA ni nafuu ukilinganisha na maji ya kununua kutoka sehemu nyingine au kupitia visima ambavyo havina uhakika wa ubora wake. Niwaombe mjitokeze kwa wingi kupata huduma ambayo ni mkombozi mkubwa kwa Wananchi hususani akina mama" alisema.

Deus Gogomoka, ambaye ni Mwenyekiti wa Mtaa Mbwawa, aliishukuru serikali kupitia DAWASA kwa kutekeleza mradi huo katika eneo hilo ambalo lilitokana na agizo la Hayati Rais Magufuli huku akiomba Mamlaka kuangalia uwezekano wa kuunganishia Wananchi huduma ya maji kwa mkopo ili iweze kuwanufaisha wananchi wengi.

"Maji haya yalisubiriwa kwa muda mrefu, tunakumbuka tumeletewa mradi huu na Hayati Magufuli wakati wa uhai wake ambaye aliona ni muda muafaka kwa wananchi wa kata yetu kunufaika na huduma. Ombi letu kwa DAWASA ni kutufikiria juu ya kutupa huduma hii kwa mkopo au gharama nafuu zaidi ili kila mwananchi aweze kunufaika," alisema Gogomoka.

Naye Tatu Hassan alitoa pongezi kwa DAWASA kwa kutekeleza mradi huu wa maji Mbwawa akisisitiza kuwa dhamira ya kumkomboa mwanamke na changamoto za maji inaenda kumalizika.

Mradi umetekelezwa na DAWASA kupitia fedha za ndani na utanufaisha zaidi ya wakazi 6,200 katika kata ya Mbwawa na baadhi ya maeneo ya viwanda.



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), wakizibua mitaro na kusafisha mfumo wa maji taka, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Utata waibuka manispaa kulipia taa fedha za ziada

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebaini malipo ya ziada ya taa za barabarani Sh. milioni 588.45 katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Jumanne, CAG Charles Kichere, anasema alibaini kuwa taa za barabarani zilizowekwa katika barabara mbalimbali kupitia mkataba uliongiwa chini ya kipande Na. 5 zililipwa kwa viwango vya bei ya juu kuliko bei iliyokubaliwa kwenye mkataba.

Anasema hiyo ilichangiwa na usimamizi duni wa zabuni husika, hivyo kusababisha ongezeko la kiwango cha malipo kwa kila taa.

Ilikuwaje? CAG anafafanua kuwa kipengele cha 36.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba Na. LGA/085/2017/2018/W/01 ulioingiwa tarehe 8 Juni 2018 kwa Sh. 23,176,087,870 kwa muda wa miezi 18.5 kati ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara na mkandarasi kinataja kuwa:

"Hati ya makisio ya gharama za ujenzi inatumika kukokotoa bei ya mkataba; na mkandarasi atalipwa kulingana na kiwango cha kazi iliyokamilika kwa bei zilizotajwa kwenye gharama za makadirio ya vifaa kwa kila kipengele."

CAG anabainisha kuwa idadi ya vitu 8,100 vilivyomo katika gharama za makadirio ya vifaa vilivyohusishwa kwenye mkataba inaonyesha kuwa bei zilizokubalika za usambazaji, uwekaji, majaribio na kipindi cha uangalizi cha miaka mitatu, taa moja ya barabarani ni Sh. 7,500,000.

"Katika upitiaji wa malipo ya mkandarasi nilibaini kuwa taa za barabarani zililipwa kwa viwango vya bei ya juu kuliko bei iliyokubaliwa kwenye mkataba kwa Sh. 588,449,414.

"Ninapendekeza Menejimenti ya Manispaa ya Mtwara ihakikishe mkandarasi anarejesha kiasi kilicholipwa zaidi ya makubaliano ya mkataba Sh. 588,449,414," CAG anatoa hoja.

Kabla ya kuwasilishwa bungeni Jumanne wiki hii na kuwa wazi kwa umma, ripoti hiyo ya CAG ilikabidhiwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan Ikulu Chamwino Machi 30, mwaka huu.

# LATRA yatoa sababu Uber kusitisha huduma

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imesema kampuni ya teksi mtandao (Uber) imesitisha utoaji wa baadhi ya huduma nchini kutokana na kushindwa kutekeleza matakwa ya bei elekezi zilizoainishwa na mamlaka hiyo Aprili 8, mwaka huu.

Aidha, Aprili 12, mwaka huu, madereva wa teksi mtandao waliandamana hadi katika ofisi za LATRA, jijini Dar es Salaam, wakishinikiza kunyang'anywa leseni wamiliki wa teksi mtandao walioshindwa kutekeleza maagizo ya bei elekezi.

Hatua hiyo ilisababisha mamlaka hiyo kutoa siku saba kwa wamiliki hao kutoa utetezi kabla ya kuchukuliwa hatua za kiudhibiti.

Katika taarifa iliyotolewa juzi, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Gilliard Ngewe, alisema katika tangazo walilolitoa katika gazeti la serikali namba 1369 la Aprili 8, tozo inayopaswa kulipwa na dereva kwa kutumia mifumo ya teksi mtandao ni asilimia 15 ya nauli. Awali tozo hizo zilikuwa asilimia 33 suala lililokuwa likilalamikiwa na madereva husika.

Alisema hadi sasa, wamiliki wote wa mifumo ya teksi mtandao waliosajiliwa na mamlaka hiyo, wamekubali kutekeleza agizo hilo la bei elekezi isipokuwa Uber.

"Mamlaka inawakumbusha watoa huduma za usafiri zinazodhibitiwa pamoja na wamiliki wa mifumo ya teksi mtandao kuzingatia sheria na kanuni zilizopo ili kuimarisha uchumi na utengamano wa jamii ya Watanzania," alisema Ngewe. Uber ambayo imekuwa ikitoa huduma ya usafiri mkoani Dar es Salaam kwa miaka sita sasa, ilitoa taarifa kupitia ukurasa wake wa huduma kwa wateja kwamba imechukua uamuzi huo wa kusitisha kwa muda huduma za UberX, UberXL na UberX Saver nchini Tanzania.

Kampuni hiyo ilisema kanuni za sasa za usimamizi wa sekta hiyo ya usafirishaji zimejenga mazingira ambayo si rafiki kwa upande wao na kudai kuwa zimekuwa changamoto kubwa katika uendeshaji wa biashara yao, hivyo hawataendelea kutoa huduma hadi mwafaka utakapopatikana.

"Nauli elekezi iliyowekwa na LATRA imesababisha changamoto kubwa kwa mifumo kama Uber kuendelea kutoa huduma kwa wateja wetu, inakuwa ngumu kwetu kuendelea kutoa huduma, hatutaweza mpaka pale mazingira yatakapokuwa rafiki kwa sisi kuendelea kutoa huduma," ilisema.

"Tuko tayari kushirikiana na mamlaka husika na kufanya mazungumzo yatakayoleta tija na kujenga mazingira wezeshi na tutarudi kuendelea kutoa huduma baada ya kujiridhisha kwamba mazingira ya kibiashara ni rafiki," iliongeza taarifa hiyo.

Kampuni hiyo iliwaomba radhi wateja wake kwa usumbufu uliojitokeza huku ikisisitiza kwamba huo ni wakati mgumu kwao wote lakini haina maana kwamba ndio mwisho wa kila kitu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la heri Simba SC kwa Orlando Pirates kesho

**WAWAKILISHI** wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Simba, kesho Jumapili watashuka dimbani kucheza mchezo wa robo fainali na Orlando Pirates ya Afrika Kusini.

Simba ambayo ndio timu pekee kutoka ukanda wa Afrika Mashariki kuendelea kuwemo kwenye michuano hiyo, ilifuzu hatua hiyo kwa kishindo baada ya ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya US Gendarmerie ya Niger kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Katika mechi hiyo ya mwisho ya makundi, Simba ilihitaji ushindi pekee kufuzu hatua hiyo na hicho ndicho kilichotokea.

Kwa kufuzu huko, Simba inaweka rekodi ya kufuzu robo fainali mara tatu ndani ya miaka mitano, mara mbili ikiwa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Tunaipongeza Simba kwa hatua hiyo kwani inapeperusha vyema bendera ya Tanzania, na hakuna shaka sasa msimu ujao nchi itawakilishwa na timu nne kwenye michuano ya kimataifa.

Pamoja na pongezi hizo, wawakilishi hao wanatakiwa kuingia kwenye mechi hiyo ya robo fainali kwa tahadhari na umakini mkubwa pale kwenye Uwanja wa Mkapa kabla ya kurudiana Aprili 24 mjini Johannesburg.

Haitarajiwi kuwa mechi rahisi kwa vile wapinzani wao pia ni timu bora na yenye uzoefu kwenye michuano hiyo.

Hivyo Simba inahitaji kujipanga vizuri na tunaamini maandalizi ya hali ya juu yaliyofanyika wana nafasi nzuri ya kufuzu nusu fainali ya michuano hiyo, jambo ambalo hakuna shaka nchi inatamani lifikiwe.

Tunaamini Simba itaibuka na ushindi Jumapili katika mchezo huo na kinachotupa matumaini ni rekodi ambayo imejiwekea timu hiyo inapocheza nyumbani kwenye michuano hiyo na maandalizi ambayo inayafanya.

Katika suala na michuano ya kimataifa kwenye Uwanja wa Mkapa kwa Simba hatuna hofu hata kidogo, tuna uhakika itashinda.

Tuna amini kwa uzoefu wake, hatuoni kama wapinzani wao Pirates kama wataweza kupata hata bao moja kutokana na mikakati iliyopo.

Simba ni tofauti na klabu nyingi za Tanzania, hasa katika mashindano ya kimataifa, hivyo tunawahimiza mashabiki kuondoa hofu na kujitokeza kwa wingi Jumapili kwenda kuishangilia timu

Umakini unahitajika kuanzia kwa viongozi, benchi la ufundi mpaka wachezaji wenyewe.

Wakati maandalizi ya mechi hiyo yakiendelea, Shirikisho la Soka Afrika, CAF, limetoa taarifa kuwa mechi hiyo ni miongoni mwa zitakazotumia VAR (Video Assistance Referee).


Tunafahamu kuwa hilo ni jambo geni nchini, mara zote maamuzi ya VAR hutumika kwenye Ligi Kuu ya England na michuano mbalimbali ya kimataifa. Simba itakuwa ya kwanza kuonja tamu na chungu ya VAR.

Tunaimani katika maandalizi ya kuelekea mechi hiyo, benchi la ufundi litafanyia kazi hilo na wachezaji wapate kuwa na uelewa zaidi juu ya VAR.

Ni imani yetu Simba imejipanga vyema kufanya yote muhimu kuelekea mechi hiyo na hakuna shaka inayo pia nafasi ya kufanya vizuri.

Hivyo sisi Nipashe tukiwa kama wadau wakubwa wa michezo hapa nchini tunaitakia kila la heri Simba katika mchezo huo na tuna matumaini makubwa kwamba haitawaangusha Watanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Ni Ligi bora ya Simba na Yanga tu Bongo?

**NIMEKUWA** nikisoma sehemu mbalimbali kuwa Ligi ya Tanzania Bara ni ya nane kwa ubora Afrika. Inawezekana ikawa ni kweli, lakini kwangu mimi ambaye nimeshawahi kuiona ligi ya Tanzania miaka ya 1980 hadi 1990, bado inanipa shida kuamini moja kwa moja kitu hicho.

Kwangu mimi ninachoona kuwa kwa sasa Ligi Kuu Tanzania Bara ni ligi inayokua kati ya ligi mbalimbali za Afrika na imekuwa maarufu kutokana na kuonyeshwa kwenye televisheni ambapo imekuwa ikionekana maeneo makubwa ya Afrika Mashariki na Kati.

Kuwepo pia kwa baadhi ya wachezaji kutoka nje ya nchi, hasa kutoka kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kunawafanya hata mashabiki wa soka wa ukanda huo kuifuatilia sana ligi ya Tanzania, pia ushabiki uliokuwepo, na hamasa unaifanya ligi kuchangamka zaidi, tofauti na ligi za nchi nyingine za karibu kwa sasa kama vile Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi.

Yaani tunaweza kusema kuwa Ligi Tanzania Bara ni moja kati ya ligi pendwa Afrika na hata ikisemekana inashika nafasi ya nne, achilia mbali nane, hapo naweza kukubali kabisa.

Kwenye ubora inanipa shaka. Bado kama Watanzania tuna safari ndefu ninavyoona ili ligi iwe bora.

> **Yaani tunaweza kusema kuwa Ligi Tanzania Bara ni moja kati ya ligi pendwa Afrika na hata ikisemekana inashika nafasi ya nne, achilia mbali nane, hapo naweza kukubali kabisa. Kwenye ubora inanipa shaka. Bado kama Watanzania tuna safari ndefu ninavyoona ili ligi iwe bora.**

Naweza kuthubutu kusema zamani Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara ambayo kwa sasa ndiyo Ligi Kuu ilikuwa bora zaidi ya sasa.

Haiwezekani Ligi Kuu inaanza, timu za Simba na Yanga tu ndizo zinazoonekana kuusaka ubingwa na si zingine. Zilizobaki zinausaka ubingwa kwa maneno tu, lakini huwezi kuona vitendo vyovyote uwanjani vinavyoonyesha ni kweli ni timu zinazopigania ubingwa.

Hata Azam FC, timu ambayo kwa miaka ya karibuni imeonekana kujipambanua kuusaka ubingwa, lakini huoni dalili hizo.

Timu inayosaka ubingwa haiwezi kushinda mechi leo, kesho inafungwa, kesho kutwa inatoka sare na timu ndogo tu, huku zingine zikishinda mfululizo.

Nikisema hivi sina maana kuwa timu zingine nazo ziwe mabingwa, la hasha. Hata miaka ya nyuma, Simba na Yanga zimekuwa zikipokezana ubingwa wa Tanzania Bara na Muungano, ingawa ulikuwa unaingiliwa na timu zingine katikati kama Coastal Union, Pamba, Tukuyu Stars, Prisons, Mseto, Cosmopolitan, Pan African, lakini kulikuwa na ushindani mkubwa tofauti na sasa.

Ukiangalia kwa sasa Simba na Yanga zinachukua ubingwa kirahisi zaidi. Zamani wakati mwingine zililazimika kusubiri hadi mechi za mwisho ndiyo ziamue.

Sababu zimekuwa ni nyingi, ikiwemo hata waamuzi wamekuwa wakizibeba mno timu hizo kubwa kwa sasa tofauti na zamani. Wakati ule hakuna TV, lakini waamuzi walikuwa makini, tofauti sasa, waamuzi wamekuwa wakivurunda huku wakimulikwa na televisheni, lakini wapi.

Ukitaka kujua hilo, angalia timu hizi za sasa zikicheza na Simba au Yanga, zinakaa nyuma, zinahitaji zaidi sare kuliko ushindi, zikibahatika kupata bao moja, basi ni hilo hilo.

Ndiyo maana zikipata sare , wachezaji wao wanashangilia, unaweza kudhani zimetwaa ubingwa. Timu inayosaka ubingwa haiwezi kushangilia sare dhidi ya Simba au Yanga. Jiulize Simba au Yanga, kufungwa mabao 2-0, 3-0, 3-1, ilikuwa lini?

Miaka ya nyuma, Simba au Yanga kupigwa idadi hiyo ya mabao ilikuwa ni kitu cha kawaida tu, tena ikiwa na wachezaji bora kabisa wanaochezea mpaka timu za taifa, Taifa Stars.

Mfano tu, Simba iliwahi kuchapwa mabao 4-2 na Reli ya Morogoro, Yanga ikabamizwa mabao 3-0 dhidi ya Pamba, tena kwenye Uwanja wa Taifa. Zinafungwa na zinachezewa mpira. Na haikuwa mara ya kwanza mbili au tatu kufungwa na timu mbalimbali za Ligi Kuu. Hii ndiyo unaweza kusema ligi bora. Kwa hizi timu zinazoshangilia sare, zikicheza kutaka kusalia Ligi Kuu, halafu tuseme ni ligi bora. Inanipa ukakasi.

# Morogoro yatekeleza agizo la Rais la ardhi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WILAYA ya Morogoro imeanza utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la utatuzi wa migogoro ya ardhi ya muda mrefu kwenye ngazi ya wilaya kwa kuanza na tathmini na uthamini kwa wananchi wanaoishi mitaa mitatu katika kata ya Mindu, Manispaa ya Morogoro.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Albert Msando, alisema tathmini na utatuzi wa migogoro ya ardhi ya muda mrefu kati ya wananchi wa mitaa ya Kasanga, Mikoroshini na Mindu inafanyika chini ya usimamizi wa uongozi wa Bonde la Wami Ruvu ambao ndio wasimamizi wa Bwawa la Mindu.

Msando alisema Rais kupitia Kamati ya Mawaziri Wanane wa Sekta Mtambuka, aliagiza kutatua migogoro mbalimbali ya ardhi, hivyo viongozi wa wilaya kwa kutambua umuhimu wa Bwawa la Mindu kuwa ni tegemeo kwa matumizi ya maji kwa wananchi wa Manispaa, imeanza kushughulikia utatuzi huo.

Alisema mgogoro huo ulianza tangu mwaka 2006 na mpaka sasa wananchi wa mitaa hiyo wanaendelea kuishi bila amani kwa kutokuelewa hatima yao pale inapojitokeza suala la mita 500 za kisheria kuzunguka Bwawa la Mindu.

Msando alisema kuishi kwao bila ya kuwa na amani kunatokana na taarifa mbalimbali kwamba wananchi hao wanapaswa kubomolewa nyumba zao na kuondolewa katika maeneo ambayo wamekuwa wakifanya shughuli zao za kujipatia riziki na makazi.

Alisema dhana nzima ya kazi hiyo ni kuangalia athari kubwa ambazo zitaathiri mazingira, uchafuzi wa maji pamoja na athari zinazoweza kutokea endapo mafuriko na kingo za bwawa kuvunjika wananchi wataathirikaje.

Msando aliwaondoa hofu wananchi hao kuwa jambo hilo si la kuwavunjia au kuwaondoa kwa nguvu katika makazi yao na endapo watapaswa kuondoka taratibu zitafuatwa baada ya mapendekezo ya pande zote mbili pasipo kuondolewa kiholela.

# Rais Samia ateua bosi mpya MSD

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi wa viongozi watatu katika taasisi mbili huku akimteua Mavere Tukai kuwa Mtendaji Mkuu wa Bohari ya Dawa (MSD).

Katika taarifa iliyotolewa juzi na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, Tukai ni kiongozi Mkuu wa Mradi wa USAID Global Health Supply Chain Technical Assistance.

Mwingine aliyeteuliwa ni Rosemary Slaa ambaye anakuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya MSD.

Taarifa hiyo ilisema Slaa ni Ofisa Mwandamizi katika Kampuni ya PricewaterhouseCoopers (PWC).

"Rais Samia amemteua Raymond Mndolwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Mndolwa ni mtaalam wa Operesheni kampuni ya STC Construction, Dar es Salaam. Uteuzi huu unaanza mara moja," ilisema taarifa hiyo.



Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Hamdouny Mansoor (wa pili kushoto) na Mtendaji Mkuu Ofisi ya Mipaka ya Kimataifa nchini Kenya, Juster Nkoroi (kushoto), wakibadilishana hati ya makubaliano ya mpango kazi wa utekelezaji kazi ya uimarishaji mpaka wa kimataifa wa nchi hizo awamu ya pili, wilayani Tarime, mkoani Mara juzi. **PICHA: WANMM**

# Tanzania na Kenya kuendelea kushirikiana kuimarisha mipaka

**Na Munir Shemweta,** TARIME

Tanzania na Kenya zimetia saini makubaliano ya mpango kazi wa kuendelea kuimarisha mpaka wa kimataifa baina ya nchi hizo kutoka eneo la Ziwa Natron hadi Namanga mkoani Arusha.

Makubaliano hayo yalifikiwa juzi wakati wa kikao cha Kamati ya Pamoja ya Wataalamu wa Mipaka kati ya nchi hizo kilichokuwa na lengo la kupokea mawasilisho ya utekekezaji kazi za awamu ya kwanza na kuangalia namna bora ya kukamilisha awamu ya pili.

Utiaji saini ulifanyika wilayani Tarime, Mara kati ya Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Hamdouny Mansoor, na Juster Nkoroi ambaye ni Mtendaji Mkuu Ofisi ya Mipaka ya Kimataifa nchini Kenya (KIBO).

Mbali na utiaji saini makubaliano ya mpango kazi, kamati ya wataalamu wa mipaka wa Kenya na Tanzania ilitembelea mpaka wa nchi hizo maeneo ya Kirongwe wilayani Rorya kwa upande wa Tanzania na Muhuru Bay katika Kaunti ya Migori nchini Kenya pamoja na mpaka wa nchi hizo eneo la Serengeti/Masai Mara ili kukagua kazi ya uwandani na kushauri namna bora ya kuendelea na kazi zinazofuta.

Awamu ya kwanza ya uimarishají mpaka wa kimataifa wa nchi hizo ulikuwa wa kipande cha urefu wa kilomita 238 kuanzia Ziwa Victoria hadi Natron. Awamu hiyo ilikamilishwa hivi karibuni kwa kipande cha kilomita 23 kutoka Hifadhi ya Taifa ya Serengeti mkoani Mara hadi Ziwa Natron.

Katika makubaliano ya mpango kazi, utekelezaji uimarishajji mpaka wa Tanzania na Kenya awamu ya pili utaanza mwishoni Aprili, mwakani na kutarajiwa kukamilika Juni 2022 kwa kipande cha kilomita 110 kutoka Ziwa Natron hadi Namanga mkoani Arusha kufanyiwa kazi.

Wakati wa utiaji saini makubaliano ya mpango kazi, viogozi wote wawili walihimiza wataalamu wa mipaka watakaoshiriki uimarishaji mpaka wa kimataifa kuondoa tofauti zao wakati wa utekelezaji na kusisitiza kuwa uimarishaji ulenge kudumisha uhusiano mzuri na kuleta manufaa kwa Tanzania na Kenya.

Mpaka wa Tanzania na Kenya eneo la nchi kavu una ukubwa wa kilomita 758 na uimarishaji wake pamoja na mambo mengine utasaidia kuondoa baadhi ya changamoto zilizokuwa zikijotokeza kwa wananchi wanaofanya shughuli maeneo ya mipakani katika nchi hizo.

# DC akerwa na neno 'mchakato' utekelezaji miradi maendeleo

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, ameeleza kukerwa na neno mchakato katika miradi ya maendeleo na kwamba hataki kusikia neno hilo hasa kwenye fedha za miradi ambazo zimetoka serikalini.

Amesema badala ya kujitetea kwa kisingizio cha mchakato watendaji hawana budi kukamilisha miradi na kuanza kutumika kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Akizungumza juzi wakati wa ziara ya kukagua miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Moyo alisema kumekuwa na ucheleweshwaji wa ujenzi wa miradi kutokana na uzembe wa wataalam kwa kisingizio kwamba wako kwenye mchakato.

Moyo alisema fedha ambazo zimeletwa na serikali zinatakiwa zitumike kwa wakati kulingana na majukumu ambayo yanatakiwa kutekelezwa kulingana na thamani ya fedha ambazo zimetolewa kwenye miradi husika.

Alisema fedha zikiwa zinaletwa kwenye miradi halafu hazitumiki kwenye miradi kwa wakati zitaleta doa kwa halmashauri husika na kushindwa kupewa fedha nyingine kwa ajili ya kutekeleza miradi mingine.

Moyo aliwataka wataalam na makandarasi kubadilika katika utendaji wao wa kazi ili kuendana na kasi ya serikali katika jitihada za kuwaletea wananchi maendeleo.

Aidha, Moyo alikemea vitendo vya baadhi ya wananchi kuiba vifaa vya ujenzi jambo ambalo alisema linarudisha nyuma maendeleo ya ujenzi, hivyo serikali ya wilaya haitamvumia mtu yeyote atakayehujumu miradi.

Kwa mujibu wa Moyo, miradi yote inatekelezwa kwa ajili ya kusaidia juu za wananchi katika kujikwamua kiuchumi na kuleta maendeleo katika maeneo husika ambako miradi inatekelezwa.

Alisema miradi yote inatakiwa kutekelezwa usiku na mchana kwa kuwa fedha zipo na zimetolewa kwa wakati kwenye miradi husika na kutekeleza miradi hiyo kwa wakati.

Moyo aliwataka wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato ya ndani ambavyo vitasaidia kuchochea maendeleo ya wananchi katika halmashauri husika.

Kaimu Mhandisi Ujenzi Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Nicolus Kasililika, alisema wameyapokea maagizo yote ya kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya ya Iringa na kuahidi kuyafanyia kazi kwenye miradi yote inayotekelezwa katika halmashauri.

Mhandisi Kasililika alisema kamati ya ulinzi na usalama imetembelea miradi mitano inayotekelezwa kwa kutumia fedha kutoka serikali kuu yenye lengo la kuchochea maendeleo kwa wananchi.

# ARU yazindua kituo utafiti na mafunzo

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO Kikuu Ardhi (ARU) kimezindua Kituo cha Utafiti na Mafunzo cha Kuimarisha Miji ambacho kinafadhiliwa na serikali ya Ubelgiji.

Serikali ya Ubelgiji imefadhili uendeshaji wa kituo hicho kwa miaka 10 kwa gharama ya Euro milioni sita, ni sawa na Sh. bilioni 15 za Kitanzania.

Uzinduzi wa kituo hicho ulifanyika jana chuoni hapo na mgeni rasmi alikuwa Balozi wa Ubelgiji nchini, Peter Van Acker, na Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Profesa Evaristo Liwa. Profesa Liwa alisema kituo hicho kitafanya utafiti kwenye maeneo mbalimbali ambayo chuo cha ARU wamebobea ikiwa ni jitihada za kupata ufumbuzi wa matatizo mbalimbali.

Alitaja baadhi ya mambo yatakayofanyiwa utafiti kuwa ni ujenzi wa nyumba, masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) na yanayolenga kuboresha huduma mbalimbali katika Jiji la Dar es Salaam kama vile usafiri mazingira maji na upangaji wa miji.

"Kutakuwa na program ambazo watu wetu kutoka hapa wataenda kuonana na wananchi na vile vile wengine watakuwa wanakuja hapa kujisomea hapahapa chuoni na pia ARU itaihusisha sekta binafsi kuendesha mafunzo," alisema.

"Kwenye hili sisi ARU ndio tunaongoza hii taasisi ila tumewashirikisha wenzetu kama Chuo Kikuu cha Nelson Mandela, Mzumbe na Tengeru," alisema Profesa Liwa. Alisema vyuo vingi vya nchini Ubelgiji vitashiriki kwenye program hiyo kupitia mpango wa kubadilishana wanafunzi wa nchi hizo mbili.

Profesa Liwa alisema kupitia kituo hicho, wanafunzi wa chuo hicho watapata shahada za uzamili (masters) na Shahada za Uzamivu (PhD) ambazo watasoma kwa pamoja na kwa wakati mmoja hapa Tanzania na Ubelgiji. "Kitu pekee ambacho kitaonekana kitakwimu kwenye mpango huu ni idadi ya shahada za uzamili na shahada za uzamivu (PhD) ambazo tutakuwa tumezitoa na wanafunzi hawataenda kusoma Ubelgiji, watafundishwa kwa pamoja hapa na kule anayehitimu anapata shahada mbili moja ya hapa moja ya Ubelgiji kwa hiyo anakuwa na shahada mbili," alisema.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo, Balozi Acker alisema anafuraha kubwa kuzindua kituo hicho ambacho anaamini kitakuwa miongoni mwa vituo mahiri.

Balozi huyo alisema ana matumaini kwamba kituo hicho kitakuwa na manufaa makubwa kituo hicho kitasaidia hata nchi za Afrika Mashariki kwa watu wao kuja kujifunza kuhusu changamoto mbalimbali za maeneo ya mijini.

"Ni matumaini yangu kwamba nchi za Burundi, Rwanda, Uganda, DRC , Kenya, Uganda watakuja kujifunmza namna ya kukabiliana na changamoto nyingi za maeneo ya mijini," alisema

"Naamini mtashirikiana na taasisi zingine za serikali kuwafikia wananchi wengi kuwapa elimu kuhusu namna ya kutatua changamoto za mijini na watu wanamatumaini makubwa sana na chuo cha ARU hivyo nawatakia mafanikio mema," alisema Balozi.



Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto (wa tatu kushoto), akimkabidhi funguo za pikipiki ya magurudumu matatu aina ya Toyo, Elizabeth Mwita ambaye ni dereva wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Kipunguni, jijini humo juzi, iliyotolewa na AMREF, kwa ajili ya kubebea malighafi za kuzalisha mkaa mbadala katika kiwanda kinachomilikiwa na kituo hicho. Kushoto ni Mkurugenzi wa kituo hicho, Seleman Bishagazi na Ofisa Masoko wa kiwanda, Tausi Msangi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Meya ataka ubunifu uzalishaji mkaa

**Na Sabato Kasika**

MEYA wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto, amewataka wakazi wa jiji kuendelea kubuni mbinu mbalimbali ambazo zitasaidia kuzalisha mkaa mbadala ili kuepuka uharibifu wa mazingira.

Kumbilamoto alisema hayo juzi wakati akikabidhi pikipiki aina ya Toyo katika Kituo cha Taarifa na Maarifa cha Kipunguni kwa ajili ya kusomba malighafi za kuzalisha mkaa mbadala katika kiwanda kinachomilikiwa na kituo hicho.

Alisema kila mwaka takriban hekta milioni moja za miti ambazo ni sawa na asilimia 70 zinakatwa kwa ajili ya mkaa, na kwamba kutokana na hali hiyo, nchi inaendelea kubaki jangwa.

Alisema takwimu za Wakala wa Huduma ya Misitu Tanzania (TFS), zinaonyesha kuwa mahitaji ya nishati hiyo nchini yanafikia tani milioni mbili hadi tatu kwa mwaka, na kwamba ili kuzalisha tani moja ya mkaa, zinahitajika mita za ujazo 10 hadi 12 za miti.

"Kulingana na utafiti wa TFS, Dar es Salaam pekee huingizwa magunia zaidi ya 500,000 ya mkaa kila mwezi, hivyo mradi wenu huu utasaidia kupunguza ukataji miti kulinda mazingira, na ungefaa kuigwa ili kunusuru mazingira," alisema Mstahiki Meya.

Alisema mbali na kunusuru mazingira, mradi wa uzalishaji wa mkaa katika kituo hicho utasaidia kupunguza magonjwa na pia utapunguzia jiji gharama za kusafirisha taka kwenda dampo.

"Lakini pia mradi huu utaokoa pesa za kununua magari maalum ya kusomba taka na utaongeza ajira, hivyo ingekuwa ni vyema kama wengine wataiga ubunifu kama wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Kipunguni," alisema.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Seleman Bishagazi, alisema mkaa wanaozalisha unaotokana na taka mbalimbali ikiwamo vifuu vya nazi, maboksi nyasi, majani ya miti na vumbi la mbao ambavyo vyote huchanganywa pamoja.

"Tunachanganya na kuchoma kwenye tanuru kisha tunachukua mchanganyiko huo na kuuwekea uji wa mhogo na kusagwa pamoja kisha tunafinyanga vipande vya mkaa kulingana na saizi tunayoitaka," alisema Bishagazi.

Bishagazi alifafanua kuwa baada ya hapo, vipande hivyo vya mkaa vinaanikwa juani kwa siku tatu au nne, na kwamba baada ya hapo unakuwa tayari kutumika.

"Tulishafanya majaribio hayo, lakini kwa kuwa sasa tumepata Toyo, kwa ajili ya kusomba malighafi za kuzalisha mkaa huu, tuko tayari kuanza biashara ya kuzalisha mkaa mbadala," alisema.

Alisema, mashine na Toyo amepewa msaada na AMREF baada ya kupata mafunzo ya ujasiriamali katika semina za kila Jumatano zinazoendeshwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

"AMREF iliona juhudi zetu na kutoa msaada wa mashine ya kuzalisha mkaa Januari mwaka huu kisha Machi ikatoa Toyo ambayo Meya ametukabidhi rasmi, nasi tulishafundisha vijana wa kiume na wa kike wa kituo hiki jinsi ya kuchakata mkaa kwa mashine na pia kuendesha Toyo," alisema.

# Watu 176 mbaroni tuhuma za uhalifu

**Na Julieth Mkireri,**
KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linawashikilia watu 176 kwa tuhuma za kuhusika na matukio mbalimbali ya uhalifu kati yao 45 ni wahamiaji haramu.

Taarifa iliyotolewa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, ilisema jana kuwa watuhumiwa hao walikamatwa katika oparesheni za kuzuia na kupambana na uhalifu zilizofanyika katika mkoa huo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, katika oparesheni hiyo vitu mbalimbali vilikamatwa pamoja na watuhumiwa hao ambavyo ni televisheni, simu za mkononi, vifaa vya ujenzi, pombe haramu ya gongo na bangi.

Kamanda Lutumo alisema watuhumiwa hao tayari wamechukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani kujibu mashitaka yanayowakabili.

Pia katika taarifa yake, Kamanda amewakumbusha wazazi kuelekea sikukuu ya Pasaka kuwa makini na watoto wao hasa wanapowapatia magari kujiridhisha ili kuepuka ajali za barabarani.

"Kuelekea sikukuu ya Pasaka, vijana wengi hupenda kufurahia sikukuu kwa kutumia dawa za kulevya na vilevi vilivyopitiliza, hivyo tunawaomba wazazi wawe makini wanapowapatia watoto wao magari," alisema.

Aliwakumbusha wenye kumbi za starehe kuweka taratibu za ulinzi wa watoto na usalama wao endapo kutakuwa na disko.

Alisisitiza kuwa Jeshi la Polisi limejipanga katika kukabiliana na matukio ya uhalifu na uvunjifu wa amani hususani katika kipindi hiki cha sikukuu na kuongeza umakini wa ukaguzi wa magari na doria katika fukwe.





# Mbunge ataka mapitio sheria mitaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kufanya mapitio ya Sheria ya Tawala za Mikoa ya mwaka 1997 ili kuangalia muundo wa sasa wa sekretarieti za mikoa unaokidhi mahitaji yaliyopo kwa sasa.Akichangia juzi hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa mwaka 2022/23 bungeni, Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, alisema:

"Tulitegemea kwenye sekretarieti za mikoa kuwe na wabobezi ili wakienda wakashauri lakini changamoto iliyopo sasa hivi sekretarieti hazina wataalamu hao unakuta mtaalamu anayekwenda kushauri ni junior kuliko anayemkuta kwenye Halmashauri unakuta ushauri wake hausikilizwi lakini hata cha kushauri hana."

Alibainisha kuwa kukiwa na mfumo imara wa sekretarieti hizo, mawaziri wataacha kukimbizana kwenye halmashauri kukagua miradi. Akizungumzia kuhusu utekelezaji wa mradi wa uboreshaji miundombinu kwenye majiji (TACTIC), alishauri masoko yajengwe kwenye maeneo yenye watu ili miradi hiyo iwe na tija kwa wananchi.

"Namshukuru Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan) kwa kuingiza Halmashauri ya Mji wa Nanyamba katika mradi huu tupo kwenye miji 45 na tunasubiri sana kwa hamu. Nikuombe Waziri (Innocent Bashungwa) tusifanye makosa yaliyopita huko nyuma miradi hii tujenge kulingana na mahitaji ya sasa, Rais ameelekeza masoko yafuate watu na si watu wafuate masoko," alisema.

Kuhusu maandiko ya miradi ya kimkakati, Chikota aliitaka TAMISEMI kuharakisha upitishaji wa maandiko hayo ya halmashauri ili kupata fedha za kutekeleza miradi hiyo kwa wakati.

"Kuna tatizo la ucheleweshaji wa maandiko asilimia 32 ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya kimkakati ndio zimetumika ina maana maandiko hayapitishwi kwa wakati, maandiko mengine yanahitaji maamuzi ya muda mchache," alisema.

Alitolea mfano mamlaka za serikali za mitaa za mikoa ya Lindi na Mtwara nyingi zimeomba kujenga maghala ya kuhifadhi korosho kutokana na mikoa hiyo kulima zao hilo lakini hadi sasa bado hayajapitishwa.

"Tupunguze halmashauri kutegemea serikali kuu. Tungeruhusu halmashauri hizi kujenga maghala kwa kuwa takribani kila Halmashauri ingepata Sh. milioni 500 kila mwaka,"alisema.



Mkulima wa Parachichi Kijiji Cha Igoda, wilaya ya Mufindi, mkoani Iringa, Paschal Chengula (kulia), akifundisha jinsi ya kupandikiza mche bora wa parachichi kwa wanufaika wa mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM), wakati wa mafunzo ya siku 10, wilayani humo, jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Mradi wawajengea uelewa wananchi kuhusu ufuatiliaji miradi Maendeleo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

UTEKELEZAJI wa mradi wa kuwajengea uwezo wananchi na asasi za kiraia mbinu na uwezo wa kufuatilia rasilimali za umma (PETS) hususan sekta ya maji, umewaongezea uelewa wa kutambua wajibu wao na kushiriki ipasavyo kwenye miradi wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma.

Ofisa Mradi wa Mtandao wa Asasi za Kiraia Mkoa wa Dodoma (NGONEDO) , Luhaga Makunja, aliyasema hayo jana alipokuwa akitoa tathmini ya mradi huo unaotekelezwa kata za Kigwe na Babayu wilayani humo kwa ufadhili wa The Foundation For Civil Society (FCS).

Alisema kupitia mradi huo uelewa wa wananchi katika kufuatilia raslimali za umma hususan maji umeongezeka ambapo wanashiriki kwenye kuibua miradi na pale inapotekelezwa waitunze ili iwe endelevu.

Makunja alisema kuanzia mwaka 2019 , NGONEDO ilikuwa ikitekeleza mradi katika Wilaya ya Bahi ili wananchi wafuatilie fedha za umma ambapo awali mradi ulitekelezwa kwenye kata za Bahi, Mpamantwa, Mundemu na Msisi na vijiji vinne vya Bahi, Mkakatika,Mchito na Nguji.

Alibainisha kuwa wananchi wanataka kushirikishwa katika upangaji wa bajeti na hata kuchangia miradi inayotakiwa kutekelezwa katika maeneo yao kulingana na vipaumbele vyao.

"Kabla ya mradi wananchi walikuwa hawapati taarifa za mradi , baada ya mradi kulikuwa na ongezeko la upatikanaji wa taarifa kwa wananchi jambo lililoongeza uwajibikaji wa viongozi kwa wananchi," alisema Makunja.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Kigwe, Jeremiah Sobayii, alisema wananchi wamejifunza namna na kutambua ubora wa usimamizi wa rasimali za umma.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Bahi, Awadhi Maega, alisema wananchi wa vijiji vya Kigwe na Asanje wamefaidika na mradi huo na matokeo yanaonekana kutokana na kufuatilia miradi inayotekelezwa katika maeneo yao.

Awali, Mratibu wa NGONEDO, Edward Mbogo, alisema mradi huo umeongeza uwezo wa kiwango cha ushiriki wa jamii katika ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma ili kuboresha utoaji wa huduma katika sekta ya maji.

Alisema mradi huo pia umesaidia kukuza uwajibikaji na uwazi wa Mamlaka za Maji Vijijini na Wilayani katika utoaji wa huduma za maji.

## Waziri awa mbogo utoroshaji madini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Dk. Doto Biteko, amekitaka Chama cha Wafanyabiashara wa Kati wa Madini Tanzania (CHAMATA) kuwa mabalozi kwa wafanyabiashara wenzao kuacha kutorosha madini.

Dk. Biteko alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na viongozi wa chama hicho alipokutana nao jijini hapa kwa lengo la ukuaji na usimamizi wa sekta ndogo ya biashara ya madini.

Alisema kuna wafanyabishara ambao sio waaminifu wanaofanya utoroshaji wa madini na kwamba Serikali imeweka Masoko ya Madini ili kuondoa urasimu.

"Rais Samia Suluhu Hassan akiwa Mwanza aliagiza watu wapeleke madini yao kwenye masoko kutoka sehemu yoyote na wauze bila kusumbuliwa. Ninataka kutumia nafasi hii kuwaomba wale wote tuliopewa dhamana ya kusimamia sekta ya madini wale watu ambao wanapeleka madini sokoni wasisumbuliwe.

"Naomba mtu asipate msukosuko, aone raha ya kwenda sokoni na soko liwe mahali pa kimbilio la wachimbaji, "alisisitiza.

Hata hivyo, waziri huyo alisema wizara imekuwa ikikutana na wadau wote wa sekta ya madini kupitia maonyesho mbalimbali ya madini na mikutano inayofanyika hapa nchini ili kuwasikiliza na kuzungumza nao kuhusu kero zinazowakabili na kuzipatia ufumbuzi.

"Wizara inatarajia kuendelea kukutana na makundi maalum mbalimbali ili kuwasikiliza na kutatua changamoto kwa pamoja. Nawataka CHAMATA mshikamane kwenye umoja huu ili kuwa na sauti ya pamoja kama ilivyo kwa vyama vingine vilivyopo katika sekta ya madini," alisema.

Naye Mwenyekiti wa CHAMATA, Jeremia Kituyo, alisema chama hicho kinataka kuona sekta ya madini inakuwa na mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa ili Tanzania inufaike ipasavyo na rasilimali ya madini nchini.

Aidha, Kituyo aliishukuru wizara kwa uanzishwaji wa masoko ya madini ambayo yamekuwa na mchango mkubwa kwa wafanyabiashara nchini.



# Mwinyi asisitiza uhamasishaji ushiriki mashindano ya Quraan

Na Mwandishi Wetu

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka Waislamu kuendelea kuhamasishana kushiriki katika mashindano ya Quraan katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani ili kupata fadhila kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo katika nasaha zake kwa washiriki wa mashindano makuu ya saba ya Quraan Tajweed Zanzibar, yaliyofanyika Masjid Nooor Muhammad Kwamchina, jijini Zanzibar.

Alisema kuna umuhimu mkubwa kwa Waislamu kuhamasishana kushirki katika mashindano mbalimbali katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani ikiwamo ya tahfidh quraan na mashindano mengineyo, kwa kuwa kuna fadhila kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Dk. Mwinyi alipongeza Ofisi ya Mufti kwa kazi nzuri inayofanya ya kuratibu mashindano mbalimbali, hivyo akatoa wito wa kuhakikisha inashirikiana na taasisi zote na kuziwezesha ili kufanikisha malengo hayo.

Pia aliishukuru taasisi ya Majlisul Quraan kwa kuandaa mashindano hayo na kutaka kuendelea na utaratibu huo kila mwaka , ikiwa ni hatua ya kuwapa uzoefu vijana ili hatimaye waweze kuiwakilisha Zanzibar kimataifa.

"Niwaombe mwendelee kuandaa mashindano haya kila mwaka na pale mnapoandaa msiache kuwaalika majaji hawa kutoka nje," alisema.

Alisema mashindano hayo ambayo yamewahusisha majaji kutoka nchi mbalimbali zikiwamo Bangladesh, Kenya na Misri, yamefanikiwa na majaji hao wameonyesha namna bora ya kuisoma Quraan, huku akisisitiza umuhimu wa vijana kuendelea kujifunza ili kuliwakilisha vyema taifa katika mashindano ya kimataifa.

Naye Mufti Mkuu wa Zanzibar, Samahat Sheikh Saleh Omar Kaab, aliwakumbusha Waislamu wajibu walionao wa kuisoma, kuifahamu na kuizingatia Quraan ili kuwapeleka mbele katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Aidha, Katibu wa Mufti wa Zanzibar, Sheikh Khalid Mfaume, alisema hatua ya washiriki wa mashindano hayo pamoja na majaji kutoka nje ya nchi kuisoma Quraan kwa ufasaha na sauti nzuri ni kitendo cha kufuata maelekezo ya Mtume Muhammad (SAW).

Mapema, akisoma risala ya Taasisi ya Majlisul Quraan, Sheikh Mohamed Kombo alisema taasisi hiyo iliyoanzishwa mwaka 1994 imepata mafanikio makubwa, lengo likiwa kuwawezesha Waislamu kuisoma na kuifundisha Quraan kama ilivyopokewa.

Alisema katika kufikia lengo la kuanzishwa kwake, taasisi hiyo imeendeleza mashindano hayo kila mwaka na kuiwezesha Zanzibar kutoa mshiriki katika mashindano makubwa yanayofanyika Tanzania, ambapo mwaka huu yatafanyika jijini Dar es Salaam April 16.

"Kiu kubwa ya taasisi ni kuhakikisha Zanzibar inapata nafasi ya kushiriki katika mashindano yanayofanyika katika nchi mbalimnbali za nje, ikiwamo Iran", alisema.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi akimkabidhi zawadi mshindi wa kwanza wa mashindano makuu ya 7 ya kusoma Quran Tajweed Zanzibar, yalioandaliwa na Majlisul Quran Zanzibar, katika Masjid Noor Muhammad Mombasa kwa Mchina, jana. Kushoto ni Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kaab. **PICHA: IKULU**

## Ujenzi soko kunufaisha wavuvi

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Masoud Suleiman Makame, amesema kukamilika kwa ujenzi wa soko la Malindi na eneo la Diko kutatoa fursa nbalimbali kwa wananchi.

Akifungua kikao cha majadiliano ya maendeleo ya ujenzi wa soko hilo kilichofanyika mjini hapo, Waziri Masoud alisema mradi huo unafadhiliwa na serikali ya Japan kupitia shirika lake la kimataifa (JICA) kwa kushirikiana na serikali ya Zanzibar kwa kutoa dola milioni moja.

Masoud alisema kwa sasa hali ya ujenzi inaenda vizuri na matarajio ni kuona ujenzi unamalizika kwa wakati ingawa awali ulisimama kutokana na UVIKO - 19 lakini sasa unaendelea katika hali nzuri na soko hilo litakuwa la kisasa kulinganisha na awali mazingira yake hayakuwa rafiki.

Naye mshauri elekekezi wa mradi huo, Ogawa Tadashi, alisema wana matumaini makubwa kukamilisha ujenzi huo Agosti, mwaka huu na ujenzi unaendelea vizuri.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema kukamilika kwa mradi huo kunakwenda sambamba na sera ya uchumi wa bluu kwa kuwa wananchi wa Zanzibar wanatarajia kufaidika na soko hilo.

Mkurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti, Sheha Idrissa Hamdani, kutoka Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi, alisema soko hilo lina fursa nyingi na wavuvi wataendeleza shughuli zao za asili walizokuwa wakifanya awali za kushusha samaki kutoka maeneo mbalimbali ya Zanzibar.

# Wazawa wamimika eneo la uwekezaji

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

BAADHI ya wawekezaji wazawa wameanza kujitokeza kwa ajili ya kuanzisha shughuli katika eneo la uwekezaji Kijiji cha Pangatupu mkoa wa Kaskazini Unguja.

Akizungumza katika eneo hilo, mwekezaji Ussi Salumu Pondeza alisema kitendo cha serikali kulitenga eneo hilo kwa ajili ya uwekezaji, kimewafurahisha wawekezaji wengi, hivyo kampuni yake inakusudia kulitumia kuanzisha kiwanda kinachozalisha malighafi za ujenzi.

Ussi alisema kwa sasa yuko tayari na anakusudia kuanza shughuli zake katika kipindi cha miezi sita baada ya kukamilisha hatua za mwisho serikalini

Alisema kiwanda hicho kitatoa kipaumbele cha ajira kwa wananchi wazawa wa mkoa huo na kuwaomba wananchi kujitokeza kwa wingi pindi kiwanda kitakapoanza shughuli za uzalishaji.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud alisema kwa sasa serikali iko katika hatua za kuimarisha miundombinu katika eneo hilo ikiwamo barabara, umeme na huduma ya maji, hivyo akawataka wawekezaji kujitokeza kwa wingi kwa ajili ya kuwekeza.


Alisema eneo hilo litakuwa na usalama wa kutosha na serikali inakusudia kujenga kituo cha zimamoto na kituo cha polisi ili kuimarisha ulinzi kwa wawekezaji pamoja na mali zao.

Alisema hadi sasa wameshajitokeza wawekezaji 10 wenye nia ya kuwekeza katika eneo hilo ambao wanakusudia kujenga viwanda vya rangi, mapambo na kuendesha shughuli zao kupitia mwongozo kutoka Wizara ya Viwanda na Maendeleo ya Biashara.

Mkuu wa Mkoa alisema serikali imeamua kulitenga eneo hilo kwa ajili ya uwekezaji kwa lengo la kuongeza fursa za ajira kwa wananchi pamoja na kukua kwa uchumi wa taifa.

Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini B Unguja, Hamid Seif Said, alifurahishwa na hatua ya mwekezaji huyo na kusema uwekezaji ni sekta muhimu kwa maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Aliwataka wananchi katika mkoa huo hasa wale wanaoishi karibu na eneo la uwekezaji kuitumia vyema fursa hiyo ili kujikwamua kiuchumi.



**RUBBY**

UKURASA 12



Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE



# MAUNDA KAMALIZA MWENDO

## Vilio, huzuni vyatawala kwa wasanii wa kike

LEO ni siku ngumu kwa familia, ndugu, marafiki wa mwanamuziki wa Bongofleva, Maunda Zorro, kwani atapumzishwa katika makazi yake ya milele baada ya kufariki kwa ajali ya gari.

Maunda Zorro aliyefariki kwa ajali ya gari eneo la Kigamboni, usiku wa kuamkia Alhamisi, atazikwa katika makaburi ya Kongowe mkoani Dar es Salaam.

Mastaa mbalimbali wa kike wamejitokeza kuonyesha majonzi yao kutokana na msiba huo. Wengi walijitokeza kuandika ujumbe mbalimbali wa kuomboleza na wengine baada ya kusikia taarifa hiyo walienda moja kwa moja nyumbani kwa baba wa marehemu Zahir Ally Zorro, eneo la Kisota.

Msanii wa filamu Monalisa, alionekana kushindwa kujizuia kulia akisema kabla yake alikutana naye ni kama alikuwa akimuaga.

Wema Sepetu kupitia ukurasa wa Instagram ameandika “Daaaaaah.... Umeniuma Maunda! Dada mzuri mwenye roho nzuri....lala kwa amani babe, njia yetu sote,”

Kwa upande wa Shilole, ameandika haya akionyesha majonzi yake “Mungu akupe kauli thabiti Maunda wangu daaaah!! “

Baadhi ya wasanii waliofika nyumbani kwa marehemu walisema watamkumbuka kutokana na tabia yake ya ucheshi, upendo na kutobagua watu.

BASI SAWA

## Jamani mwacheni Harmorapa

RAPA Harmorapa, ambaye umaarufu wake umeshuka kwa kasi ameamua kumuachia Mungu kwa kile walichokifanya Chidi Benz na Q Chief, kuhusu yeye.



Hivi karibuni, Chid Benzi na Q Chief, katika ukurasa wa Instagram walionekana kujadili muonekano mpya wa Harmorapa na kusema maneno ambayo yalionekana kwake kama kumdhalilisha.

"Chidi Benz na Q Chief wameshindwa kuzuia mihemko yao. Mbarikiwe na ninawapenda sana watu wangu wa mfano, Chuma na Chila ahsanteni kwa kejeli na vicheko vyenu". Ameandika Harmorapa

## Rhino King angalia umechokoza nyuki

MASHABIKI na wafuasi wa mwanamuziki wa Bongo Fleva, Harmonize, wamemjia juu Rhino King, wakisema asitumie jina la msanii huyo kupata umaarufu.

Hayo yamekuja baada ya Harmonize kuweka video katika ukurasa wake wa Instagram, akionekana akifundishwa mchezo wa ngumi, kisha akaomba mtu yeyote mwenye matatizo naye binafsi basi wakamalizane ulingoni.

Rhino King alimjibu kupitia akaunti yake ya Instagram kuwa yupo tayari kwa pambano hilo.

Kutokana na jibu hilo, wafuasi wa Harmonize, wameeleza Rhino King hana ubavu wa kushindana na mwanamuziki huyo kwani anachokifanya sasa ni kutaka umaarufu.






## Maskini Ruby bado kabisaa

BADO kuna utata kuhusu afya ya mwanamuziki wa kike Ruby Andrea Wayayu, ambaye ameibua mjadala kutokana na andiko lake la kuomba afe mapema.

Meneja wa mwanamuziki huyo, amesema wameamua kumfanyia ushauri msanii huyo kutokana na changamoto mbalimbali za kimaisha zinazomkabili kwa sasa.

"Ni changamoto za dunia tu zimetokea, wala sio kiki ila ni kweli hayuko sawa kwa sasa. Mungu ni mwema anaendelea vizuri, tumemuomba akae kwanza ili kujipumzisha," amesema meneja huyo.



## Dullyvani kwa hilo unaliweza

MCHEKESHAJI Dullvani, amejigamba kwamba nyota yake inang'aa kwa wanawake na huko ndipo anajipatia pesa nyingi kuliko wasanii wengine.

Akizungumza na Planet Bongo ya East Africa Radio, Dullvani amesema kuigiza kama mwanamke ni jambo gumu lakini inamnufaisha kutokana na wasanii wengine kuhofia kuingia katika sanaa ya aina hiyo.

"Kila mtu siku hizi anaigiza kama mwanamke anavaa madera lakini mimi ndio nimefanya iwe hivyo, nimeifanya jamii iamini kuigiza kama mwanamke ni uhusika  tu, na sio kitu kingine," amesema.

## MAANA YA MITINDO YA BENDI ZA DANSI

**Na Adam Fungamwango**

BENDI nyingi za muziki wa dansi huwa na mitindo yake. Ziwe bendi za zamani au za kisasa, kila bendi utasikia inatumia mtindo fulani. Mfano African Stars wao mtindo wao ni 'Twanga Pepeta' Ni jina ambalo limekuwa maarufu sana na kufunika hata jina la bendi yenyewe.

Diamond Sound wao wanajiita wana 'Ikibinda Nkoi', African Revolution wao awali kabisa mtindo wao ulikuwa ni 'chumvi chumvi tutalamba', lakini baadaye wakabadilisha na kuiita 'Tamtam'.

Tukirudi nyuma zaidi, bendi nyingi zilitumia mitindo hiyo wakiwa na maana mbalimbali. Lakini mara nyingi zilikuwa ni aina za ngoma za makabila ya Kitanzania.

Leo tutaangalia mitindo ya bendi mbalimbali kuanzia miaka ya 1970, hadi 1990 na maana na kwa nini waliamua kujiita hivyo.

**Saboso-Western Jazz**

Bendi ya Western Jazz, moja ya bendi kongwe nchini tangu miaka ya 1960, ilitumia mtindo wa 'Saboso'. Bendi hii ndiyo iliyopiga nyimbo kadhaa maarufu kama 'Vigelegele', 'Roza', 'Jela ya Mapenzi', 'Nilikupenda Sana', na nyingine nyingi walitumia mtindo huo ulioletwa na mmoja wa wanamuziki wa bendi hiyo, ikiwa ni jina la ngoma za moja ya makabila ya mkoa wa Singida.

**Msondo Ngoma-Juwata Jazz**

Kwa sasa jina la mtindo limegeuzwa kuwa la bendi. Bendi hii kongwe na maarufu nchini, iliazishwa mwaka 1964 ikiitwa Nuta Jazz, ikiwa na mtindo wa 'Kiwelewele'. Lakini baadaye ukabadilishwa na kuwa 'Msondo Ngoma'. Hata ilipobadilishwa majina, ikawa Juwata Jazz, Ottu Jazz, bado mtindo ulikuwa huo huo, hadi ilipoondoka chini ya umiliki wa Vyama Vya Wafanyakazi Tanzania, na wanamuziki wakaanza kujitegemea wenyewe, ndipo jina la mtindo likawa la bendi na kuwa Msondo Ngoma Music. Muhidini Mwalimu Gurumo, ndiye aliyetoa jina hilo. Ni jina la ngoma ya Kizaramo ya unyago, ambayo hutumika kuwacheza na kuwafunda wasichana wanawari.

**Sikinde - DDC Mlimani Park.**

Hapa tunakuta mzee Gurumo tena. Baada ya kutoka Msondo kwenye Orchestra Mlimani Park, mwaka 1978, aliasisi mtindo wa 'Sikinde Ngoma ya Ukae'. Maana yake ni sikinde ngoma ya nyumbani kwa lugha yake ya asili ya Kizaramo, kama alivyoipa Juwata jina la Msondo. Sikinde pia ni moja kati ya ngoma za kabila hilo la kizaramo.

**Super Bomboka-Dar International**

Marijani Rajab alikuwa moja wa waanzilishi wa bendi ya Dar International. Hata hivyo alikuwa chini ya uongozi wa Abel Bathazal mwaka 1977. Kukatokea mgogoro, Marijani akatimuliwa. Mwaka mmoja baadaye Bathazal na karibia asilimia 90 ya wanamuziki wa bendi hiyo wakaenda kuunda bendi mpya ya Orchestra Mlimani Park. Mmiliki wa bendi akaenda kumuangukia Marijani arejee kuisuka upya bendi. Akawa yeye ndiye kiongozi. Anaipa mtindo wa 'Super Bomboka'. Maana yake ni bomu lililopasuka. Yaani ukweli wa nani mzuri, nani mbaya umejulikana.

**Ogelea Piga Mbizi-Maquiz Original**

Maquiz Du Zaire ni moja kati ya bendi chache ambazo walikuwa wakibadili mitindo mara kwa mara. Walianza na 'Chakula Chakula Kabombe', wakaja na 'Kamanyola bila Jasho', baadaye 'Sanifu', halafu 'Ogelea Piga Mbizi' wakiwataka mashabiki wake kucheza kama wanaogelea na kupiga mbizi. Wapinzani wao OSS walipotangaza kutumia mtindo wa "Chunusi Madoido',  wakiwatisha wote wanaoogelea baharini, kuwa wataliwa au kupotezwa na mdudu huyo wa kufikirika, wakabadili mtindo na kuwa 'Zebwela', ambalo ni neno la Kizaramo likiwa na maana kutembea au kuzurura.

## Kwetu Uswazi: ukiyakuta yaache huku huku

**Na Adam Fungamwango**

LEO tunaitazama filamu ya  'Kwetu Uswazi', iliyochanganyika na ucheshi kidogo kutokana na aina ya waigizaji kama kina mzee Majuto na mzee Jengua ambao wote ni marehemu. Pia kwenye filamu yupo mzee Msisiri.

Inaanza kwa kuonyesha kuwa mzee Majuto na kijana wake Kinye Mkali wakizozana kutokana na wote kuwa na tabia mbaya ya kuchukua wanawake hovyo.

Imefikia wakati wanawake wa mzee Majuto ndiyo hao hao wa kijana wake Kinye Mkali, hivyo kuanza kuzozana wenyewe kwa wenyewe.

Jirani yao mmoja mlevi anafika nyumbani kwa mzee Majuto na kumuonya juu ya kutembea na mkewe.

Mkewe Majuto naye anakwenda nyumbani kwa mke wa mlevi huyo na kumpiga mkwara juu ya kutembea na mumewe.

Upande wa pili nako, mzee Msisiri ana wake wawili. Lakini wake zake hao wote wana uhusiano wa kimapenzi na kijana wa mzee Majuto, Kinye Mkali.

Habari hizo zikafika mpaka kwa mzee Msisiri mwenyewe kwa sababu walikuwa wakigombana mara kwa mara juu yake,  na akaapa kumfanyia kitu kibaya.

Kwa mzee Jengua nako, wanaume kibao wanajitokeza kutaka kumposa binti yake, lakini anakataa.

Vijana wa kiume wakifika hapo, yeye anawatoa mbio.

Ikaja kufahamika kuwa mzee huyo ana uhusiano wa kimapenzi na binti yake.

Binti akaanza kuwa na kiburi kwa mama yake, huku mama akiwa hajui ni kwa sababu gani.

Siku moja shemeji wa mzee Jengua ambaye ni kaka wa mkewe, akawafuma laivu wakikumbatiana, akawa amepata jibu la kwa nini hataki binti aolewe.

Mzee Msisiri anamfanyia mambo ya kishirikina Kinye Mkali na anaanza kuwa chizi.

Matatizo ya akili ya mtoto wa Majuto yanasababisha wake za mzee huyo kumrudia mumewe na kumuomba msamaha. Ni kwa sababu hawawezi tena kuwa na uhusiano na mtu mwenye shida ya afya ya akili.

Mzee Msisiri aliwasamehe wake zake na kuwaruhusu kurejea nyumbani.Shemeji wa mzee Jengua anakwenda polisi kushtaki kuwa mzee




huyo anatembea na binti yake, kiasi cha kukataa asiolewe. Askari wanafika nyumbani na kumkamata mzee huyo na kupelekwa kituoni kwenye kujibu tuhuma hizo.




# JLo mapenzi hadi kwenye jakuzi

MWANAMUZIKI mkongwe wa Marekani, Jennifer Lopez, amewekа wazi kuwa amechumbiwa na Ben Affleck wakati wakioga katika jakuzi.

Akihojiwa katika jarida moja, JLo amesema kwa sasa wana mahaba mazito licha tangu uhusiano wao kuwa rasmi siku hiyo.

"Usiku wa Jumapili tukiwa sehemu ya dunia namaanisha jakuzi, penzi tamu lilielekea katika ndoa na hapo alinichumbia," amesema JLo.



## Temi, Mr Eazi kufunga ndoa?

WANAMUZIKI nyota wa Nigeria, Temi Otedola na Mr Eazi, wanatarajia kuwa mke na mume baada ya wawili hao kuchumbiana rasmi.

Nyota hao walichapisha picha wakiwa pamoja wiki hii, huku Mr Eazi, akisema hawezi kulala vizuri akikumbuka siku hiyo.

Uhusiano wa kimapenzi kati ya Mr Eazi na Temi umekuwa kivutio kwa watu wengi na imesababisha kuongeza umaarufu katika sekta ya burudani.

## Piga makofi kwa Britney Spears

MWANAMUZIKI kutoka Marekani, Britney Spears, na mume wake Sam Asgharigot, wanatarajia kupata mtoto wao wa kwanza.

Wawili hao walichumbiana mwaka 2021, waliweka posti katika mtandao wa Instagram wakiwa taarifu mashabiki wao kuwa wanatarajiwa kuwa wazazi.

"Nimepunguza uzito wakati nikitafta kurudi tena, ingawa ndugu zangu kuna kitu kinatokea tumboni mwangu, mume wangu aliniambia kuna chakula cha mtoto. Nimekwenda kupima nina ujauzito," ameandika Britney.





## TI Blaze si bure kuna jambo tu

MWIMBAJI maarufu kutoka Nigeria, TI Blaze, amekamatwa na polisi kutokana na kosa ambalo halijafahamika.

Kulingana na mmoja wa watu wanaofanya kazi katika kundi lake, TI Blaze amekamatwa Jumanne amekamatwa na polisi mmoja wa kiume.

Mwanamuziki huyo baadae alindika katika ukurasa wake wa Instagram kwamba amekamatwa kutokana na madai ya kutishia kuuwa.

## Kelvyn Boy kumbe unakataa mtoto

MARAFIKI wa karibu wa mwimbaji Kelvyn Boy, wamesema msanii huyo anatuhumiwa kukataa ujauzito wa mwanamke mmoja raia wa Marekani.

Kulingana na mtoa taarifa hiyo Esther Abrefi Owusu, Kelvyn Boy, amemtelekeza mwanamke huyo kwa muda mrefu na kwenda kuishi kwa mpenzi wake mpya wa kike aliyemzidi umri.

Amesema anayajua vizuri maisha ya mwanamuziki huyo raia wa Ghana, na kwamba kitendo cha kumtelekeza mwanamke mwenye ujauzito ni sawa na unyama pamoja na kumfanyia unyanyasaji wa nyumbani.



# DAWASA KAZI INAENDELEA

## ■Wabunge wasifu utekelezaji wa miradi Dar, Pwani
## ■Maji yamwagika Chalinze wananchi ni vicheko tu

**Na Mwandishi Wetu**




Rais Samia Suluhu Hassan, akizundua mradi mkubwa wa maji wa Mlandizi-Chalinze hivi karibuni

HIVI karibuni kamati tatu za kudumu za Bunge zilitembelea Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kuangalia miradi inayotekelezwa na mamlaka hiyo kama inalingana na thamani ya fedha zinazotolewa na hatua zilizofikiwa kwenye utekelezaji.

Kamati hizo ni Kamati ya Bunge, Kilimo, Uvuvi na Maji, Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji (PIC), ambazo kwa kiwango kikubwa zilielezea kufurahishwa na ulinganifu wa thamani ya fedha na utekelezaji wa miradi hiyo.

Wabunge wameridhishwa na utendaji wa kazi katika kubuni na kusimamia miradi mbalimbali ya maji huku wakitaka kuongeza kasi na usimamizi ili ifikapo mwaka 2025, huduma hiyo ifikie asilimia 95 ndani ya Jiji la Dar es Salaam na miji ya Mkoa wa Pwani.

Kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ilitembelea miradi ya Maji Makongo - Bagamoyo na mradi wa Mkuranga ambayo imekamilika na inatoa huduma kwa wakazi waliokusudiwa.

Wakiwa katika mradi wa maji Mkuranga, Kamati iliagiza Mamlaka kuhakikisha kuwa awamu ya pili ya mradi huo inayolenga kufikisha maji kwa wakazi wa Vikindu hadi Kongowe inatekelezwa.

Mradi wa maji Mkuranga awamu ya kwanza umetekelezwa kwa gharama ya Shilingi bilioni 5.5. Chanzo cha maji ya mradi huo ni kisima cha maji chenye kina cha mita 545 chenye uwezo wa kuzalisha lita 284,400 kwa saa.

Kwa sasa mradi huo unahudumia wakazi mji wa Mkuranga waliopo katika kata za Kiparag'anda kwenye mitaa ya Mkuranga A, Mkuranga B, Kiguza, Mgawa, Bigwa, Mkwalia - Kitumbo, Njia Nne na Sunguvuni huku wateja 2,154 wakiwa wameunganishiwa huduma ya maji kupitia mradi huu.

Makamu Mwenyekiti wa PAC, Japhet Hasunga (Mb) amesema mradi wa maji Mkuranga umetekelezwa kwa ufanisi na wameridhika na kazi iliyofanyika.

"Tumetembelea mradi na tumeona kazi iliyofanyika, tumeridhika kusikia wananchi wanapata maji kutoka kwenye chanzo hiki," anasema Hasunga

"Ni wakati sasa kwa Menejimenti ya DAWASA kujenga tenki lililokusudiwa eneo la Mwanambaya ili wananchi wa vitongoji vilivyo jirani na Mkuranga ikiwemo Mwanambaya, Vikindu mpaka Kongowe wapate huduma ya maji ya kuaminika." anaongeza Hasunga

Kamati hiyo pia ilitembelea mradi wa ujenzi wa mfumo wa usambazaji maji kutoka katika kata ya Makongo mkoani Dar es Salaam hadi mjini Bagamoyo unaogharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 65.

Hata hivyo, wabunge hao walionyesha kuridhishwa na utekelezaji wa maradi huo ambao unahusisha ujenzi wa matenki matatu makubwa yatakayowahudumia wakazi zaidi ya 450,000.

"Sisi kama kamati ya Bunge tumefanya ziara hii ili kuona na kutathmini thamani ya fedha zilizotolewa na Serikali katika miradi mbalimbali, nikiri kwamba tumeridhishwa na kazi zilizotekelezwa na DAWASA na kila mmoja wetu amejionea umakini wa kazi iliyofanyika hali inayosababisha kuona uwiano wake na thamani ya fedha ," anaeleza Hasunga.

Aidha, Hasunga ameongeza kuwa lengo la ziara ilikuwa kuona namna Bodi ya Wakurugenzi inavyowajibika katika kusimamia fedha na miradi kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya Serikali.

Mradi huu unatekelezwa kupitia fedha za wadau wa maendeleo na kusimamiwa na DAWASA kwa gharama ya kiasi cha Shilingi Bilioni 64. Utakapokamilika utahudumia wakazi wa maeneo ya Changanyikeni, Vikawe, Goba, Bunju, Madale, Wazo, Ocean Bay, Salasala na sehemu ya mji wa Bagamoyo.

Akipokea maagizo hayo, Jenerali mstaafu Davis Mwamunyange amewashukuru wabunge kwa ushauri wao mzuri wenye tija kwa Mamlaka hiyo, na pia anasema mojawapo ya siri ya kufanikiwa katika utekelezaji wa miradi ya maji ni kutokana na uongozi mzuri.

"Tunafurahi kuona kamati imeridhika na kazi kubwa tunaiyofanya ya usimamizi wa fedha na utekelezaji wa miradi kwa thamani halisi ya hela, hii inatutia moyo sana na tunawaahidi uwajibikaji zaidi ili kufikia malengo yaliyowekwa" anasema Jenerali mstaafu Mwamunyange

Kwa upande wa wabunge wanaounda kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji (PIC), Mwenyekiti wake, Jerry Slaa anasema hali ya usambazaji maji katika Jiji la Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani inaridhisha hususani maeneo yaliyokuwa na changamoto ya upatikanaji wa maji kama vile Kisarawe na Pugu.

"Mfano mzuri ni katika jimbo la Ukonga, ambapo kwa takribani miaka 40 hapakuwepo huduma ya majisafi, lakini utekelezaji wa mradi wa Pugu-Gongo la Mboto umemaliza changamoto hiyo iliyodumu kwa muda mrefu," anasema Silaa

Silaa anasema kwa kasi wanayoenda nayo DAWASA ifikapo 2025, itakuwa imewafikia wananchi wote katika eneo lake la kihuduma la Dar es Salaam na Pwani.

Kwa upande wake, Ofisa Mtendaji Mkuu DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja, anasema kazi kubwa imefanyika na inaendelea kufanyika, katika usambazaji wa maji ili kuhakikisha yanawafikia wananchi wote.

"Tumepokea maelekezo kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan kuharakisha usambazaji wa maji kwa wananchi katika maeneo ambayo miradi imekamilika, na tunashukuru wabunge kujiridhisha na utekelezaji wake na tumepokea maelekezo yao katika kuharakisha usambazaji wa huduma ya maji" anasema Mhandisi Luhemeja

Bakari Utingo, mkazi wa Kata ya Majohe yeye anasema anashukuru kwa kupata huduma ya maji katika kata zote za Pugu na kwa sasa maji ni mengi na ya uhakika.

"Nakumbuka mara ya mwisho maji kutoka bombani katika kata yetu ya Majohe tulipata mwaka 1999, tumekuwa tukitumia maji ya visima na kununua kwa watoa huduma binafsi kwa muda mrefu. Tunashukuru kwa sasa kupata huduma hii muhimu waendelee na kasi ya kuunganisha kwa wananchi wengi zaidi," anasema Utingo

### KIGAMBONI KAZI INAENDELEA

Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, anasema Wizara yake imepatiwa fedha za kutosha na serikali ili kuhakikisha huduma ya majisafi inafika kwa watu wote wa Kigamboni.

Mhandisi Maryprisca, anatoa ahadi hiyo mbele ya wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge Kilimo, Mifugo na Maji iliyotembelea mradi mkubwa wa Maji wa Kigamboni - Kimbiji.

Anasema, Mradi wa maji Kigamboni ni mfano wa miradi ambayo serikali imetoa fedha shilingi bilioni 25 kwa lengo la kukamilisha ili uweze kutoa huduma kwa wakazi wa Kigamboni ambao awali hawakuwa na chanzo cha uhakika cha maji.

Naye Mwenyekiti wa Kamati, Christina Ishengoma, anasema kamati imetembelea mradi na imeridhika na hatua nzuri iliyofikiwa ya utekelezwaji, kamati inaelekeza mradi ukamilishwe ifikapo Juni mwaka huu.

"Tumejionea mradi umetekelezwa kwa viwango na hakuna mjumbe mwenye hoja tofauti," anasema Ishengoma.

### CHALINZE NI KICHEKO

Wabunge hao pia walipata fursa ya kutembelea mradi wa maji Mlandizi - Chalinze - Mboga ambao ulizinduliwa na Rais Samia hivi karibuni.

Mradi huo ambao umekamilika, ulizinduliwa kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Maji Duniani, Machi 22, 2022.

Mhandisi Cyprian Luhemeja, anasema mradi huo ulianza kutekelezwa mwaka 2019 na hadi unakamilika umegharimu kiasi cha bilioni 18.

"Chalinze ilikuwa na changamoto ya upatikanaji wa maji, walikuwa wanapata kwa mgao, masaa nane au matano au wanakosa kabisa kwa wiki nzima, lakini kukamilika kwa mradi huu kutaleta sura mpya," anasema Mhandisi Luhemeja.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, akiwa ameambatana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji katika ziara hiyo anatoa maagizo kwa DAWASA ya kuwarudishia wateja sugu huduma ya maji kwa makubaliano maalum.

Wateja hao ni wale waliositishiwa huduma kutokana na madeni makubwa na kusisitiza wapewe nafasi ya mazungumzo na kuingia makubaliano ya kisheria ili nao wafurahie huduma hiyo.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAPOELEKEA

# Fasheni ya kupiga 'chata', na 'panchi' ukutani ilivyosumbua

## ●Mpiga chata, ofisi ya 'ticha mkuu' aibuka

Na Adam Fungamwango




KILA kitu kinawenda kwa fasheni, iwe nzuri au mbaya, mfano ni aghalabu kwa miaka ya sasa kuona maandishi yasiyo rasmi yameandikwa sehemu mbalimbali kama vile kwenye kuta za shule za msingi, sekondari na hata vyuo, ikiwemo vyooni. Wakati mwingine hata kwenye siti za mabasi.

Maandishi mengine utayakuta kwenye madeski ya kukalia wanafunzi, kwenye masinki ya vyooni. Pia kuta za viwanja mbalimbali vya soka, viwanda na sehemu mbalimbali ambazo wakati mwingine unashangaa hata huyo aliyendika alipanda vipi juu kwenda kuandika maneno hayo.

Ilikuwa ni kama aina fulani ya fasheni ya watoto na vijana wa wakati huo, ambayo ilionekana kutamatika katikati ya miaka ya 1990. Kuna wanaosema walikuwa ni wahuni waliokuwa wakifanya hivyo. Lakini wengine wanajiuliza, kama ni hivyo kwa nini maandishi hayo yaliandikwa hata kwenye shule za msingi, sekondari au vyuoni, tena hadi kwenye madawati? Jibu likaja kuwa ilikuwa ni fasheni tu ya vijana wa wakati huo, ambayo ikaigwa na watoto.

Maandishi hayo wenyewe wakayatafutia majina, wakayaita 'chata'. Wengine wakaita 'panchi'.

Kuna aina ya kwanza ya chata ni kuandika maneno ya kulaumu uongozi wa shule, viwanda kama kuna maonevu yoyote yale kwa wanafunzi au wafanyakazi, au kutoa ujumbe mkuu.

Wanafunzi wanaweza kuamka na kukuta sehemu moja imendikwa kuwa wanafunzi wamechoka na chakula kibovu.

Mshangao ni kwamba sehemu iliyoandikwa maneno hayo inakuwa si rahisi kufikika, lakini si sehemu iliyojificha, hivyo kushindwa kujulikana ni kwa nini hata walinzi hawajamuona mtu huyo.

Hata sehemu za viwandani, mfano maeneo ya Pugu Road na sehemu zingine miaka ya 1970 hadi 1980, wafanyakazi wanaweza kufika na kukuta kuna mtu ameandika mlalamiko ya wafanyakazi ambayo huwa wanayalalamikia kwa siri juu ya uongozi wao. Maandishi hayo yameandika juu kabisa ya ukuta wa kiwanda, eneo ambalo lina taa na zinamulika na walinzi wapo, lakini wakashindwa kumuona.

Hata maandishi hayo yanapofutwa, inabidi wafutaji watafute ngazi na watu wanakuwa si mmoja, ni wawili na kuendelea kwenda kufuta hayo maandishi. Na mara nyingi hayafutiki hivi hivi, bali ni kwa kupaka rangi.

Cha ajabu ni kwamba hadi leo haikujulikana walikua wanaandikia kwa kalamu, rangi au kitu gani.

Pili ni kwamba hakuna taarifa yoyote tangu wakati huo, ambayo tumewahi kusikia watu hao maarufu kama 'panchi' au 'chata', wamekamatwa. Kwa ufupi hawajawahi kukamatwa.

Aina ya pili ni ya wale watu ambao huwa wanapenda tu watoto wa mjini wanaita 'ujiko'. Yaani kujitangaza na inaonekana kwao kama ni kama burudani tu.

Hawa ndiyo wazee wa 'chata'.

Kuna hadithi moja huko Temeke kuwa watu walipoamka asubuhi walikutana na chata moja kubwa kwenye bango moja juu, ambalo lilikuwa karibu kabisa na tansifoma ya umeme.

Bango hilo jinsi lilivyokaa ilikuwa ni ngumu kujua yule jamaa aliyandika alipanda vipi, akaandika 'Lando'.

Kwa watu walioishi Wilaya ya Temeke miaka ya 1970, hadi 1980, wala si jina geni kwani alikuwa anapiga chata zake nyingi maeneo mengi ya majengo mbalimbali kuanzia Chang'ombe, Temeke, Tandika na sehemu mbalimbali.

Kilichokuwa kinawashangaza wengi ni kwamba huandika kwa kitu kile kile anachoandikia kila siku. Saizi ya maandishi ni ile ile na hata jinsi ya uandishi wa herufi zake huwa ni huo huo. Hakosei hata kidogo.

Hii ni kwamba huwa hatumi mtu, ni yeye ndiye anayezunguka kote. Huwa ni saa ngapi anafanya kazi hiyo haijulikani.

Wakati naiwasilisha mada hii kwenye mtandao wa kijamii, kuna watu wameniandikia mengi, wakikumbuka zamani.

Mmoja alisema kuwa alikutana na mwanafunzi mwenzake waliosoma miaka ya 1970, sasa ni bosi mkubwa tu. Akamtania aende akafute chata yake aliyoiweka shuleni wakati wanamaliza darasa la saba, LY.

Mwingine ananiambia zamani ukikutana na chata iliyoandikwa 'Mtoto Six', ujue ye kwake hiyo.

Mchangiaji mwingine kutoka Mwadui, yeye akasema wakati anamaliza shule aliandika LY Cool.

Mmoja aliyesoma Rungwe, akadai kuna mtu alikuwa anajii ya Jims Cultureman alikuwa kiboko kwa kutembeza chata zake.

Yupo aliyesoma shule ya Sekondari Sengerema, akasema kuwa aliweka chata zake za 'complex' kwa rangi nyeupe hadi kwenye ofisi ya mwalimu mkuu, pamoja na kutafutwa sana, lakini hadi anamaliza, hakujulikana.

Kuna jamaa alikuwa akichora maeneo 'Mgodo Mgodiki alikuwepo', mwingine 'MC Chogo alikuwa hapa'.

Kuna huyu mwingine akaniandikia kuwa kipindi hicho kwenye mabasi ya Mbeya kwenda Kyela, alikuwa ampiga 'chata' sana kwenye mabasi hasa ya Stranger, na alikuwa akiandika 'Kapalampya alikaa hapa.'

**Tuma meseji 0716 350534.**

## HABARI KIMATAIFA

# VITA UKRAINE YAZIDI KUWAKA

## ■Russia yapoteza meli vita iliyozama baharini
## ■Yatishia kusogeza nyuklia katikati ya ulaya



Papa Francis akiongoza ibada takatifu ya Ijumaa Kuu katika kanisa la Mt. Peter Basilica, Vatican jana. **PICHA: REUTER**

**KYIV,** UKRAINE

MELI ya kivita ya Russia ambayo iliharibiwa na mlipuko siku ya Jumatano imezama, wizara ya ulinzi ya Russia imesema.

Wizara hiyo ilitoa ujumbe uliosema kwamba meli ya Moskva ambayo ni muhimu kwa Russia katikati ya Bahari Nyeusi, ilikuwa ikivutwa kwenda bandarini, lakini dhoruba iliyotokea baharini ilisababisha kuzama.

Meli hiyo ya kubeba makombora na wafanyakazi 510 ilikuwa ishara ya nguvu za kijeshi za Russia, ilikuwa ikiongoza mashambulizi ya majini dhidi ya Ukraine.

Ukraine ilisema makombora yake yaligonga meli hiyo ya kivita.Hata hivyo upande wa pili haujaripoti shambulio lolote. Hata hivyo ilithibitisha chombo kilizama baada ya moto kutokea ndani.

Taarifa hiyo ilisema moto huo ulisababisha mlipuko wa risasi zilizohifadhiwa ndani ya meli hiyo ya kivita, lakini wafanyakazi wote walihamishwa hadi kwenye meli za karibu zilizokuwa katika Bahari Nyeusi.

Awali Russia ilikana kwamba meli hiyo ilikuwa ikizama na badala yake Alhamisi jioni vyombo vya habari vya serikali vilitangaza Moskva imepotea.

"Wakati wakiivuta kuelekea bandari iliyokusudiwa, meli hiyo ilipoteza usawa wake kutokana na uharibifu uliokuwa ndani ya meli wakati moto ulipozuka baada ya risasi kulipuka. Kutokana na hali ya bahari iliyochafuka, meli ilizama," shirika la habari la serikali Tass lilinukuu Wizara ya Ulinzi ya Russia.

Maofisa wa kijeshi wa Ukraine, walisema waliipiga Moskva kwa makombora ya Neptune yaliyotengenezwa na Ukraine .

Silaha hiyo iliundwa baada ya Russia kutwaa eneo la Crimea mwaka 2014, na kuwa tishio kwa Ukraine katika Bahari Nyeusi.

Ofisa mkuu wa Ukraine, alisema kuwa wafanyakazi 510 wanahofiwa kuwa ndani ya Moskva.

Katika siku ya kwanza ya uvamizi nchini Ukraine Februari 24, Moskva ilipata sifa mbaya baada ya kukiteketeza kikosi kidogo cha askari wa mpaka wa Ukraine wanaolinda Kisiwa cha Snake katika Bahari Nyeusi.

Meli hiyo ilijengwa katika enzi ya Soviet, ilianza kufanya kazi miaka ya 1980. Iliwekwa chini katika mji wa kusini mwa Ukraine wa Mykolaiv, ambao umeshambuliwa kwa bomu na Russia katika siku za hivi karibuni.

**RUSSIA YATISHIA KUTUMIA NYUKLIA**

Rais wa Russia Vladimir Putin, ameotoa onyo kwa NATO kwamba ikiwa Sweden na Finland zitajiunga na muungano wa kijeshi unaoongozwa na Marekani, nchi hiyo itapeleka silaha za nyuklia na makombora ya hypersonic katikati ya Ulaya.

Finland, ambayo inapakana na Russia ukubwa wa kilomita 1,300 sawa na maili 810 na Uswidi zinafikiria kujiunga na muungano wa NATO.

Dmitry Medvedev, Naibu Mwenyekiti wa Baraza la Usalama la Russia, alisema kuwa, iwapo Sweden na Finland zitajiunga na NATO, basi Russia italazimika kuimarisha vikosi vyake vya nchi kavu, majini na anga katika Bahari ya Baltic.

Medvedev pia aliibua kwa uwazi tishio la nyuklia siku ya Alhamisi kwa kusema kwamba hakuwezi kuwa na mazungumzo zaidi ya Baltic isiyo na nyuklia ambapo Russia ina eneo lake la Kaliningrad kati ya Poland na Lithuania.

"Hatuwezi kuwa na mazungumzo zaidi ya hali ya kutokuwa na nyuklia kwa Baltic na usawa lazima urejeshwe," alisema Medvedev, ambaye alikuwa rais wa Russia kutoka 2008 hadi 2012 alisema.

Medvedev alisema anatumai Finland na Uswisi hazitajiunga na NATO. Ikiwa sivyo, watalazimika kuishi na silaha za nyuklia na makombora ya hypersonic karibu na nchi hizo.

Russia ina hazina kubwa zaidi ya silaha za nyuklia, nchi zingine ni China na Marekani.

Msemaji wa Ikulu ya Kremlin Dmitry Peskov, aliulizwa kuhusu maoni ya Medvedev na waandishi wa habari, yeye alijibu

"Hili limezungumzwa mara nyingi na Rais Vladimir Putin ametoa amri juu ya kuimarisha upande wetu wa magharibi kutokana na uwezo wa kijeshi wa NATO unaokua,"

Alipoulizwa ikiwa uimarishaji huu utajumuisha silaha za nyuklia, Peskov alisema, "Siwezi kusema kutakuwa na orodha nzima ya hatua muhimu. Hili litashughulikiwa katika mkutano tofauti na rais."

Lithuania ilisema vitisho vya Russia si jambo jipya na kwamba ilikuwa imepeleka silaha za nyuklia Kaliningrad muda mrefu kabla ya vita vya Ukraine.

**UKRAINE KUKABILIWA NA CHANGAMOTO KUBWA**

Vikosi vya Ukraine vitakabiliwa na changamoto kubwa mashariki mwa nchi hiyo, ambako wanajeshi wa Russia wanakusanyika kwa ajili ya shambulio jipya.

Kulingana na mkurugenzi wa zamani wa CIA, David Petraeus, alisema hii ni mara ya kwanza wakati wa vita hiyo kuona Warussia wakikusanya juhudi zao zote katika eneo moja badala ya kuzunguka nchi nzima.

"Kwa hiyo, ikiwa hali ya hewa ni nzuri kwao, maeneo yakiwa makavu na wanaweza kupeleka magari kwenye maeneo hayo basi wanaweza kupanga safu ya magari katika maeneo hayo". Alisema.

Sababu nyingine itakuwa jinsi msaada wa ziada wa usalama unaweza kufikia Ukraine haraka.

Aliongeza kuwa inaonekana Rais Vladimir Putin hapendi kushiriki katika mazungumzo hivi sasa, na anataka mafanikio yanayoonekana kusherehekea kabla ya Mei 9 wakati gwaride la kila mwaka la Siku ya Ushindi wa Vita vya Pili vya Dunia huko Moscow.

**MUINGEREZA ALIYEPIGANA UKRAINE AONEKANA**

Picha na video zimeibuka kwenye kituo cha habari cha Russia akionekana Muingereza ambaye alikuwa akipigana na vikosi vya Ukraine huko Mariupol.

Aiden Aslin kutoka Nottinghamshire, alionyeshwa akiwa amezuiliwa kwa pingu, baada ya kuiambia familia yake siku ya Jumanne kwamba kikosi chake kinajiandaa kujisalimisha kwa vikosi vya Russia.

Mama yake Ang Wood alisema anaamini kuwa ni yeye kwenye picha hiyo, pia alitaka atendewe kwa mujibu wa mikataba ya Geneva.

"Tunatumai kuwa labda kunaweza kuwa na aina fulani ya kubadilishana wafungwa. Hatujui ni nini kingine cha kufanya hivi sasa isipokuwa kuendelea kushinikiza ofisi ya kigeni." Alisema.

# MATUKIO YA IBADA YA IJUMAA KUU



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akishiriki Ibada ya Ijumaa Kuu katika Kanisa Katoliki Parokia ya Maria Theresa Ledochowska, kiwanja cha ndege, jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**



Vijana wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Azania Front, wakifanya igizo la mateso na kusulubiwa kwa Yesu Kristo, wakati wa Ibada ya Ijumaa Kuu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Vijana wakifanya igizo la mateso na kusulubiwa kwa Yesu Kristo katika Usharika wa Azania Front, wakati wa Ibada ya Ijumaa Kuu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Sehemu ya waumini waliohudhuria Ibada hiyo katika Usharika wa Azania Front. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Kijana Andrea Clement, akiigiza mateso ya Yesu Kristo, katika ibada ya Ijumaa Kuu, kwenye Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria Mpalizwa Mkwawa, mjini Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**



Mchungaji wa Kanisa la Anglikana mtaa wa Madaba, wilayani Muheza, mkoani Tanga, Paulo Luhinga (kulia), akiendesha ibada ya Ijumaa Kuu katika kanisa hilo, jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo aliusimamia msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# Kama ipo, ipo tu-1

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




ILISIKIKA sauti ya kufoka kama chatu. Waliokuwa wakiongea wakaacha. "Nini hicho jamani?" Mmoja akauliza. "Hata wewe umesikia Mage?" Mwingine akauliza "Ndiyo."

"Mbona mimi sijasikia kitu?" mwingine akauliza. Hata walivyokuwa wakiulizana hazikuwa sauti kubwa. Walikuwa wananong'ona. Wananong'ona kwa hofu.

Lilikuwa ni kundi la wasichana sita waliokuwa wakitoka kuchota maji kisimani. Walikuwa wakifika hatua chache tu kutoka kwenye barabara kuu ya Segera, itokayo Chalinze kwenda Tanga na Arusha.

Ikabidi wanyamaze, halafu wasikilize tena kama kulikuwa na sauti inayofanana na waliyoisikia.

Kwa sasa ilisikika vizuri zaidi. "Siyo chatu huyo?" Mage alinong'ona. Nusura watupe ndoo zao chini ili wakimbie.

"Hapana Mpaje, chatu hafoki hivyo, wala tusikimbie, huyo siyo chatu, hebu tuangalie ni nini?"

Kwa kawaida wanawake wa vijijini hawana woga sana kama wa mjini. Wameshazoea kukaa vijijini na kukutana na wanyama au wadudu kama hao, na wanajua jinsi gani ya kukabiliana na vitu kama hivyo.

Wakiwa na ndoo zao za maji, walinyata kwa uangalifu kuelekea sehemu ambayo sauti ile inatoka.

Na kila walipokuwa wakizidi kupiga hatua, sauti ile ilisikika vizuri zaidi. Wale ambao hawakuwa waoga sana ndiyo waliotangulia. Walikuwa wakipekua majani, huku na kule kuangalia ni nini kinachofoka.

"Jamani mtu." Sauti ya kushtuka na mshangao kwa pamoja ilitoka kwa Mpaje. Waliobaki walisimama ghafla na kuangalia kwa makini zaidi mbele.

Walichokiona ni kitu kilicho hai. Alikuwa ni binadamu. Lakini hakuwa kwenye hali yake ya kawaida. Alikuwa amelala chini. Lakini akigalagala taratibu kama vile mtu anayetaka kukata roho.

"Aiii jamani kumbe mtu." Mwingine alidakia. "Amefanya nini?" Uoga wa kwamba alikuwa chatu uliwaondoka. Wakaanza kusogea tararibu kumuelekea mtu yule. Bado woga ulikuwepo kwa watoto wale wa kike, lakini ulipungua, kwani kumuogopa chatu, si sawa na kumuogopa binadamu. Tena akiwa hajiwezi. Amelala akihangaika.

Walichogundua kwa haraka wasichana hao ni kwamba mtu yule hakuwa mwenyeji wa pale, kwa sababu hawakumfahamu. Alikuwa anatapatapa, lakini hakuwa anaongea.

**"Kwani wewe ni nani?" Siwatu alimuuliza. Mtu yule akatikisa kichwa. Siwatu hakujua maana ya kutikisa kichwa. Lakini akajiongeza na kudhani kuwa anachojibiwa ni kwamba hawezi kuongea.**

Nguo zake zililoa damu, na kuchanika, hivyo walishindwa kujua hata rangi ya nguo hizo. "Jamani, sijui amekutana na mnyama au vipi." Mwingine alisema. "Jamani ee, twendeni tukateke maji." Mage aliwaambia wenzake.

"Wee Mage utaondokaje wakati kuna mtu hapa, anahitaji msaada huyu." "Unasikia we Siwatu, huyu mtu hata hatumjui, sijui katokea wapi na alikuwa anakwenda wapi, kwanza tutamsaidiaje sisi wanawake watupu hapa?"

"Kumsaidia yoyote anaweza kutoa msaada, tumsaidie." msichana mmoja ambaye alijulikana kwa jina la Siwatu aliwaambia wenzake ambao walionekana hawakukubaliana naye.

"Sasa huyu utamsaidia vipi, siyo mwanajiji mwenzetu, ingekuwa wa hapa, tungeweza kwenda kuwaita wanaume waje kumchukua."

"Kwani kumsaidia mtu mpaka umjue..." Siwatu akasitisha kuongea baada ya kugundua kuwa wenzake wameshapiga hatua kadhaa.

Ilimshtua, lakini haikumtisha Siwatu. Alitua ndoo yake chini. Akazidi kumsogelea mtu yule aliyeonekana ni kama mtu aliyejeruhiwa. Kwa mara ya kwanza alishuhudia mtu yule aliinua mkono juu. Ilionekana kama ishara ya kuomba msaada.

Siwatu alirudi nyuma na kuinua ndoo yake na maji akaipeleka karibu na mtu yule. Akaanza kumwagia taratibu kwa lengo la kumsafisha kutokana na damu zilizokuwa zikimtoka.

Kwa mbali aliona mtu yule akinyoosha mkono tena kama ishara ya kuhitaji kunywa maji. Alichukua kata iliyokuwa kwenye ndoo, akachota na kusogea karibu yake. Pamoja na kwamba alikuwa ana wasiwasi kwani alikuwa peke yake porini, mita chache kutoka kwenye barabara kuu, lakini huruma yake ilimeza wasiwasi wake. Miguu yake ilitetemeka kwa hofu. Akajikaza na kuinama. Sasa alikuwa akimuangalia mtu yule sura ambayo ilikuwa imetapataa damu. Alichofanya kwanza alimwagia kichwani. Akaokota majani na kumpangusa. Angalau sura ikaonekana. Akaanza kumnywesha maji. Aliweza kunywa. Alipomaliza alitingisha kichwa kuonyesha ishara ya shukurani, japo alionekana ana maumivu makali.

Inaonekana maji yale aliyomwagiwa na kunywa, yalimfanya kupata nguvu angalau.

"Kwani wewe ni nani?" Siwatu alimuuliza. Mtu yule akatikisa kichwa. Siwatu hakujua maana ya kutikisa kichwa. Lakini akajiongeza na kudhani kuwa anachojibiwa ni kwamba hawezi kuongea.

"Hawezi kuongea kwa sababu ya kuumia huku, au ni bubu?" Akajiuliza.

Hata hivyo, aliondoka na wazo ya kwamba ni bubu kwa sababu akakumbuka alimuuliza swali la "wewe ni nani", akajibiwa kwa ishara. Hiyo inaonyesha kuwa anasikia.

Mpaka hapo Siwatu hakujua nini tena afanye kwa mtu yule. Msaada gani mwingine anaotakiwa kufanya. Aliishiwa mbinu. Kama mtu yule angalau angekuwa anaongea hata kwa mbali, wangeweza kujadiliana nini cha kufanya. Akafikiri kidogo. Angalau sasa wasiwasi ulianza kumuondoka baada ya kugundua hakukuwa na hatari yoyote kama ambavyo yeye na wenzake awali walivyodhani.

"Samahani, basi naomba kwenda kijijini nikawaambie watu kama kuna mtu ili waje wakusaidie, sawa ee?" Siwatu alimwambia mtu yule.

Akaitikia kwa kichwa kukubali. Siwatu aliinua ndoo yake na kujitwisha. Asingeweza kujitwisha kwa urahisi kama ingejaa, lakini kwa wakati huo ilikuwa imebaki nusu.

Aligeuka na kumtazama yule mtu. Naye akainua tena mkono kama ishara ya shukurani. "Nitarudi, usiwe na wasiwasi." Alisema kwa sauti, akimtia matumaini.

**INAENDELEA JUMAMOSI**

# SIMBA QUEENS YATAKA KUSHINDA MECHI SITA

Na Saada Akida

KOCHA wa Simba Queens, Sebastian Nkoma amesema walijiwekea mikakati ya kushinda mechi sita za duru la pili ikiwemo dhidi ya Watani wao wa Jadi 'Yanga Princess', kwa ajili ya kutetea ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu huu.

Simba Queens juzi waliendelea kufanya vizuri ushindi wa 7-0 dhidi ya Oysterbay Queens mchezo uliopigwa, uwanja wa Uhuru Dar es Salaam.

Ushindi huo unaifanya Simba Queens kuendelea kuongoza msimamo wa Ligi hiyo wakiwa na pointi 39 baada ya kushinda mechi zote 13.

Akizungumza na gazeti hili jana, Sebastian alisema kati ya michezo sita waliyojiwekea tayari wameshinda mchezo mmoja na sasa wanajipanga kwa michezo ijayo ikiwemo dhidi ya Ilala Queens na Yanga Princess.

Alisema walishinda juzi dhidi ya Oysterbay Queens na sasa wamebakiza mechi tano ambazo wakishinda hizo watakuwa wamekusanya pointi 54.

Simba Queens inashuka dimbani Aprili 19, mwaka huu dhidi ya Ilala Queens, mchezo utakaopigwa jijini Dar es Salaam.




Mshindi wa Jackpot Bonus ya **Sportpesa** Omega Ngapesa Mapunda mkazi wa Mbinga akionyesha mfano wa Hundi ya Bonus hiyo katika ofisi za **Sportpesa jijini Dar Es Salaam.**

# Ashinda Mil 9 za Jackpot Bonus

Na Dennis Fussi

MKAZI wa Mbinga, Omega Ngapasa Mapunda, ameshinda shilingi 9,989,145 katika Jackpot Bonus ya Sportpesa iliyochezwa mwishoni mwa wiki, baada ya kupatia kwa usahihi mechi 11 kati ya mechi 13.

Akizungumza baada ya hafla ya makabidhiano ya mfano wa hundi katika ofisi za Sportpesa jijini Dar es Salaam, Omega amesema alianza kucheza na Sportpesa miaka mitatu iliyopita.

''Nilianza kucheza na Sportpesa mwaka 2019, baada ya kuwa naona kwenye mitandao ya kijamii hasa kupitia Instagram washindi wakiwa wanaonesha mfano wa hundi za kiasi walichoshinda.

Kwa mujibu wa maelezo yake, Omega amesema baada ya kuanza kucheza kwa mwaka mzima aliacha mwaka 2020, lakini baadae mwaka huu alianza kucheza tena.

"Mimi nilivutiwa na odds kubwa za Sportpesa, lakini, baada ya kutokuwa nashinda mikeka nafikiri mwaka 2020 nilisimama kucheza. Ilikuwa kuanzia Desemba, lakini mwaka huu ulipoanza nilibadili mawazo baada ya kuona kwenye Instagram washindi wakiwa na mfano wa hundi zao."

Akielezea namna alivyopata ushindi huo wa Jackpot bonus amesema mkeka alioshinda aliweka siku ya Ijumaa, lakini alianza kuuchambua tangu Jumatatu.

"Nilichambua timu tatu mpaka nne siku ya Jumatatu baadae Jumanne nikachambua timu na Alhamisi nikamalizia timu zilizobaki.

"Jumamosi usiku nilikuwa na uhakika na timu 10, hivyo Jumapili nilikuwa na shauku kubwa sana na kufanikiwa kushinda timu nyingine moja siku hiyo.

"Kwa kweli nilipagawa kidogo nilipopata ujumbe mfupi wa kunitaarifu nimeshinda Jackpot Bonus na kupigiwa simu na mtoa huduma kwa wateja. Sikulala usiku kucha nikiwazia hii fedha kwa kuwa nilianza kucheza tena mwezi wa kwanza mwaka huu".

Naye Meneja Uhusiano na Mawasiliano Sportpesa, Sabrina Msuya alimpongeza Omega kwa kushinda Jackpot Bonus ya mechi 11 na kumtaka aendelee kucheza kwani Jackpot imeshakuwa kubwa sana hivyo aendelee kuipigania pamoja na watanzania wote.

## Madam Flora atoa somo kwa wanawake

Na Sabato Kasika

NYOTA wa muziki wa Injili Madam Flora, amewataka wanaume kuacha kunyanyasa wake zao na kuongeza kuwa wanaofanya hivyo Mungu anawaona, na machozi ya wanawake hao yanakwamisha maendeleo yao.

Mwimbaji huyo ameandika hayo kwenye mitandao ya kijamii na kuwa ikitokea mwanaume anashtuka usiku hajajifunika shuka huku mkewe amejifunika, ugomvi unaanza, anampiga mkewe kwa sababu ya shuka.

'Siyo kila ndoa ni mapenzi ya Mungu, ndio nyingi ni za matamanio.Kilicha cha Mungu hata mkipishana ni rahisi kusameheana na upendo unatawala," amesema Madam Flora.

Amewataka wanawake kujitambua na kwamba wale ambao bado hawajaolewa wasikurupuke kuingia kwenye ndoa, na pia amewataka wanawake kusaidiana kukomesha vitendo hivyo katika jamii.

Madam Flora ameendelea kuweka wazi kuwa; "Ifike mahali wanawake saidieni wanawake wenzanu, usifurahi mwenzako anaponyanyaswa kijinsia maana kesho yako huijui.

Amewataka wanawake wasikubali kusubiri kufa na kuacha watoto wakiteseka na mama wa kambo, na kwamba mapenzi yapo tu, hivyo waangalie usalama wao kwanza, mengine Mungu atafanya.

'Unakuwa kwenye ndoa kwa kuigiza una furaha, lakini umejaa madonda mwili mzima kwa kipigo, kuchanwa viwembe. Mama mmoja alikuwa akipigwa na mumewe ikafika mahali akapata tatizo la akili akapelekwa wodi ya vichaa," amesema.

Mwimbaji huyo amesema mwingine alipigwa hadi akaharibiwa kizazi, hawezi kuzaa tena.Waliopata ulemavu wakiwa kwenye ndoa na wengine kufa ni wengi hawaelezeki.

## Dunga Queens wajipanga mzunguko wa pili

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

TIMU ya Dunga Queens imesema katika mzunguko wa pili wa ligi kuu ya Wanawake Zanzibar wamejipanga kuhakikisha wanapata matokeo mazuri ikilinganishwa na mzunguko wa kwanza .

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Suleiman Mohmmed amesema timu yake imepanga kuondosha uteja wa kufungwa na badala yake iweze kufanya vizuri ikiwemo kupata matokeo ya kushinda.

"Tumejipanga kupata matokeo mazuri ikilinganishwa na mzunguko wa kwanza, kulingana na timu yangu ilivyo inanibidi tuanze mazoezi mapema sana," alisema.

Aidha alisema kilichopelekea timu hiyo kufanya vibaya katika mzunguko wa kwanza ni wachezaji wake wengi kutokuwa uzoefu.

Alisema wachezaji wengi walikuwa wamezoea kucheza mashindano ya shule kwa kuwa ni wanafunzi, hivyo walikosa mbinu za kiuchezaji kwenye ligi.

Alisema kadri timu hiyo ilivyokuwa ikishuka dimbani ilibadilika na kuweza kucheza vizuri, lakini wanaendelea na kuwafundisha mbinu za kupata mabao na hata kutofungwa kirahisi.

Timu ya Dunga Queens inaburuza mkia ikiwa na alama mbili katika mechi tisa kwenye msimamo wa ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar yenye timu 10 .

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**HARRY KUTOHAMA**
MSHAMBULIAJI wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28, anatazamiwa kukacha mpango wa kuhamia Manchester United msimu huu wa joto na kusalia Tottenham, huku klabu hiyo ya Old Trafford ikitarajiwa kumtangaza Erik ten Hag. (***Mirror***)

**HAG HAMTAKI RONALDO**
ERIK Ten Hag imeweka wazi kwa uongozi wa Manchester United kwamba, mshambuliaji nyota wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, hatafaa . (***Star***)

**BERGWIJN HANUNULIWI**
ERIK Ten Hag hafikiria kumnunua winga wa Tottenham Hotspur na Uholanzi, Steven Bergwijn mwenye umri wa miaka 24, atakapochukua mikoba ya Manchester United.(***Mail***)

**AARONS AWINDWA**
MLINZI wa kulia wa Norwich, Max Aarons analengwa na Manchester United na Arsenal, wakati Bayern Munich na Borussia Dortmund pia zikimfuatilia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka miaka 20.(***Sun***)

**CARLOS ATAKIWA NEWCASTLE**
BEKI wa kati wa Sevilla, Diego Carlos mwenye umri wa miaka 29 anaweza kuwa chaguo zuri kwa Newcastle United msimu huu wa joto. (Chronicle)

**TCHOUAMENI AWANIWA**
KLABU ya Manchester City imemfanya kiungo wa kati wa Monaco, Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 22, kuwa mlengwa wao mkuu msimu huu kuchukua nafasi ya Fernandinho anayeondoka. (***Football Insider***)

**ADEYEMI ANUKIA DORTMUND**
KLABU ya Borussia Dortmund inakaribia kumnasa mshambuliaji wa Red Bull Salzburg, Karim Adeyemi mwenye umri wa miaka 20, ambaye anahusishwa na uhamisho wa kwenda Liverpool. (***Sky Germany***)

**MARTINEZ AWINDWA**
KLABU ya Tottenham Hotspur ina nia ya kumsajili Lautaro Martinez wa Inter Milan msimu huu wa joto baada ya kumkosa Januari, lakini wanatazamiwa kukabiliwa na ushindani kutoka kwa Atletico Madrid kumnunua mshambuliaji huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 24. (***Football Transfers***)

**CELSO KUBAKI SPURS**
KLABU ya Villarreal ipo wazi kwa mazungumzo na Tottenham Hotspur kuhusu uhamisho wa kudumu wa Giovani lo Celso baada ya kuwa na kiungo huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 26 kwa mkopo tangu Januari. (***Football Insider***)

**GVARDIOL KUTUA LEEDS**
LEEDS United wameongeza juhudi za kumnunua mlinzi wa Croatia, Josko Gvardiol baada ya kukaribia kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 alipoondoka Dinamo Zagreb kwenda RB Leipzig mwaka 2020. (***Football Insider***)

**MAHREZ KUONGEZA MKATABA**
KLABU ya Manchester City bado inasubiri kupokea majibu ya ofa zao za mkataba mpya kwa winga wa Algeria, Riyad Mahrez mwenye umri wa miaka 31, Raheem Sterling mwenye miaka 27 na mshambuliaji wa Brazil, Gabriel Jesus, 25. (***Teamtalk***)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LUKAKU AREJEA CHELSEA

●●●Anaweza kuivaa Crystal Palace kwenye mchezo wa nusu fainali ya FA kesho...

**LONDON, England**

THOMAS Tuchel amefarijika Chelsea kupata fursa ya kurejea kwa haraka katika nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Crystal Palace, ambayo huenda Romelu Lukaku akapatikana kwenye mchezo huo wa kesho.

Ilikuwa wiki ngumu kwa Chelsea, kwani licha ya kuonesha kiwango bora wakiwa ugenini dhidi ya Real Madrid katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hawakuweza kusonga mbele.

Wakiwa nyuma kwa mabao 3-1 kutoka kwa mechi ya nyumbani, mabingwa hao watetezi wa Ulaya walionekana kama wangefuzu nusu fainali baada ya Timo Werner kufunga bao la tatu, lakini Madrid wakajibu kwa mabao ya Rodrygo katika muda wa kawaida na Karim Benzema dakika za nyongeza.

Huku Chelsea wakiwa salama kiasi katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, lengo lao kuu sasa ni Kombe la FA.

The Blues angalau walicheza mechi ya marudiano ya Madrid bila majeraha, huku Tuchel akibainisha kabla ya mechi ya Palace kuhusu uwezekano wa kurejea kwa Lukaku.

"Romelu alirejea mazoezini jana (Alhamisi). Hebu tuone kama kuna lolote litatokea," alisema Tuchel akiwaambia waandishi wa habari.

Kocha huyo wa Chelsea atakuwa anatafuta kuweka rekodi yake nzuri ya nusu fainali, baada ya kushinda mara 11 na kutoka sare moja kati ya mechi 12 za awali kama hizo.

Na Tuchel anaamini kuwa Chelsea itafaidika kutokana na kuingizwa moja kwa moja kwenye mechi nyingine kubwa - hii ni mechi yao ya kwanza ya Kombe la FA dhidi ya mahasimu wao wa London, Palace tangu 1975-76, huku timu hizo mbili kila moja ikishinda mechi mbili kati ya nne za awali.

"Nadhani sote tuko katikati," Tuchel alisema. "Kujiamini kwa busara, nadhani ni nyongeza kubwa, lakini bado inasikitisha kutoka kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwenye robo fainali.

"Sio mchezo wa kuigiza, si kwa namna hii, lakini bado ni jambo la kukatisha tamaa sana, kwa sababu tunahisi kama tungeweza kuwa moja ya timu nne katika nusu fainali.

"Ni hisia za ajabu, kwa sababu tulikuwa na kazi kubwa ya kwenda Madrid, tukihitaji kushinda tukiwa na angalau mabao mawili ili kufikisha muda wa ziada. Tulikuwa mbele kwa mabao matatu.

"Katika mchezo wa mtoano huko Bernabeu, ni mchezo mzuri na unabaki hivi. Lakini ina ladha chungu, kwa sababu tumetoka kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya."


LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,144

MECHI KALI
MANCHESTER CITY
VERSUS
LIVERPOOL
1 | 2.53
X | 3.26
2 | 2.67

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MAN CITY WAKOMAA NA HAALAND



**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City wanaendelea kuchunguza uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Haaland, lakini kipengele chake cha kuachiwa kwa pauni milioni 63 kwa mkupuo mmoja kinaonekana kuwa kikwazo, kwa mujibu wa Sky Sport.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kipengele cha kuachiwa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 kinafaa tu hadi mwisho wa Aprili, na kuwapa City na Real Madrid tarehe ya mwisho inayokaribia kuashiria nia yao juu ya mpango huo.

City hawana wasiwasi wowote juu ya bei ya Haaland, lakini kikosi cha Pep Guardiola kingependelea kuepuka kulipa kiasi hicho kwa pamoja. Man City wanajipanga kufanya makubaliano na Dortmund ambayo yatawawezesha kulipa kidogo zaidi ya hicho, lakini kurefusha malipo kwa muda fulani.

Sehemu ya mbinu ya City inatokana na ada kubwa za wakala ambazo lazima zilipwe kwa Mino Raiola na babake Haaland.

City pia wameweka wazi kuwa hawataki kumlipa Haaland zaidi ya mchezaji anayelipwa zaidi kwa sasa Kevin De Bruyne, ambaye mkataba wake una thamani ya takriban pauni 450,000 mara tu nyongeza zitakapoongezwa.

Kuna matumaini katika Uwanja wa Etihad kwamba City wanaweza kuchukua fursa ya kutokuwa na uhakika kutoka kwa wawindaji wenzao Real.

Los Blancos wanatanguliza saini ya Kylian Mbappe na sasa wanahaha kumtafuta fowadi mwingine mwenye hadhi ya juu huku Karim Benzema mwenye umri wa miaka 34, akiendelea kucheza katika kiwango kinachokaribia kustahili Ballon d'Or.

# De Bruyne, Walker kuikosa Liverpool



**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City itawakosa Kevin De Bruyne na Kyle Walker kwenye mchezo wa nusu fainali ya kombe la FA dhidi ya Liverpool, leo.

De Bruyne alitoka nje dakika 25 kabla ya suluhu na Atletico Madrid Jumatano baada ya kuonekana kuumia kifundo cha mguu, dakika kumi kabla ya Walker naye kuumia.

Huku leo wakielekea Wembley kuwakabili wapinzani wao Liverpool, gazeti la The Times limesema kuwa kocha Pep Guardiola anajiandaa kwa mechi hiyo bila De Bruyne na Walker.

Kiungo huyo wa kati wa Ubelgiji ameondolewa kwenye mchezo huo baada ya kuonekana akiwa na barafu kwenye kifundo cha mguu wake wa kulia, ambao aliumia kufuatia teke la Felipe wa Atletico mapema kwenye mechi lakini akajaribu kucheza.

Kuhusu Walker, anaonekana kama 'shaka kubwa' kwa sababu naye ameumia kifundo cha mguu.

Joao Cancelo anatarajiwa kuwa beki wa kulia, huku Oleksandr Zinchencko akijaza upande wa kushoto.

Kwa bahati nzuri kwa City, hakuna wasiwasi wa muda mrefu kuhusu wachezaji hao wawili.

De Bruyne alikuwa akitembea bila msaada aliporejea England na haamini kuwa ameumia sana, lakini muda wa mechi ya Liverpool haujafanya kazi kwa upande wake..

## HABARI MICHEZO


,195,580

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 16/04/2022 | 17:00 | Watford vs Brentford | 2.66 | 3.16 | 2.66 |
| 02. 16/04/2022 | 17:15 | Alaves vs Rayo Vallecano | 2.57 | 3.03 | 2.93 |
| 03. 16/04/2022 | 17:30 | Manchester City vs Liverpool | 2.35 | 3.21 | 2.96 |
| 04. 16/04/2022 | 18:00 | St Etienne vs Brest | 2.31 | 3.21 | 3.11 |
| 05. 16/04/2022 | 20:00 | Dijon vs AC Ajaccio | 2.31 | 3.10 | 3.15 |
| 06. 16/04/2022 | 20:00 | Nimes vs Sochaux | 2.44 | 3.15 | 2.90 |
| 07. 16/04/2022 | 20:00 | Valenciennes vs Le Havre | 2.65 | 3.15 | 2.65 |
| 08. 17/04/2022 | 16:00 | Metz vs Clermont Foot | 2.65 | 3.15 | 2.70 |
| 09. 17/04/2022 | 16:15 | Newcastle vs Leicester | 2.50 | 3.20 | 2.80 |
| 10. 17/04/2022 | 18:30 | Union Berlin vs Eintracht Frankfurt | 2.38 | 3.26 | 2.91 |
| 11. 17/04/2022 | 20:30 | Bayer Leverkusen vs RB Leipzig | 2.71 | 3.41 | 2.46 |
| 12. 17/04/2022 | 20:30 | Giresunspor vs Besiktas | 2.88 | 3.28 | 2.36 |
| 13. 17/04/2022 | 22:00 | Sevilla FC vs Real Madrid | 3.19 | 3.19 | 2.31 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 16/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 5812 | Cagliari vs Sassuolo | 2.75 | 3.60 | 2.33 |
| 14:15 | 1660 | Hearts vs Hibernian | 1.99 | 3.22 | 3.47 |
| 14:30 | 5620 | Tottenham vs Brighton | 1.53 | 4.10 | 5.80 |
| 15:00 | 2912 | Elche vs Mallorca | 2.62 | 3.02 | 2.87 |
| 15:30 | 3852 | Udinese vs Empoli | 1.80 | 3.69 | 4.09 |
| 15:30 | 5816 | Sampdoria vs Salernitana | 1.81 | 3.71 | 4.01 |
| 16:00 | 1172 | Amazulu vs Maritzburg Utd | 2.26 | 2.83 | 3.52 |
| 16:00 | 1733 | Sekhukhune United vs TS Galaxy FC | 2.07 | 2.98 | 3.82 |
| 16:00 | 3575 | Alanyaspor vs Antalyaspor | 2.10 | 3.29 | 3.39 |
| 16:00 | 4493 | Varbergs Bois vs GIF Sundsvall | 1.78 | 3.41 | 4.09 |
| 16:00 | 5933 | Djurgardens IF vs Norrkoping | 1.71 | 3.69 | 4.08 |
| 16:00 | 5947 | Altay vs Basaksehir | 3.62 | 3.37 | 1.99 |
| 16:30 | 1009 | Augsburg vs Hertha BSC | 1.87 | 3.55 | 3.95 |
| 16:30 | 1223 | Borussia Dortmund vs VfL Wolfsburg | 1.50 | 4.62 | 5.42 |
| 16:30 | 4477 | Mainz vs Stuttgart | 2.00 | 3.49 | 3.54 |
| 16:30 | 4722 | Zenit St Petersburg vs Ural Yekaterinburg | 1.18 | 6.57 | 12.95 |
| 16:30 | 4751 | SC Freiburg vs VfL Bochum | 1.62 | 3.95 | 5.00 |
| 17:00 | 1447 | Watford vs Brentford | 2.75 | 3.19 | 2.55 |
| 17:00 | 1528 | Manchester Utd vs Norwich City | 1.28 | 5.39 | 9.89 |
| 17:00 | 2947 | Shakhter Soligorsk vs BATE Borisov | 2.22 | 3.25 | 2.91 |
| 17:00 | 3509 | Southampton vs Arsenal | 3.62 | 3.43 | 1.99 |
| 17:00 | 4012 | Partick Thisle vs Raith Rovers | 2.15 | 3.15 | 3.30 |
| 17:00 | 4887 | Morton vs Hamilton | 2.47 | 3.07 | 2.82 |
| 17:15 | 3960 | Alaves vs Rayo Vallecano | 2.67 | 3.08 | 2.77 |
| 17:30 | 1859 | Manchester City vs Liverpool | 2.53 | 3.26 | 2.67 |
| 17:30 | 3275 | Fiorentina vs Venezia | 1.35 | 4.91 | 7.82 |
| 18:00 | 2381 | TSV Hartberg vs Admira Wacker | 2.61 | 3.05 | 2.57 |
| 18:00 | 3378 | Cape Town City vs Bloemfontein Celtic | 2.27 | 2.92 | 3.36 |
| 18:00 | 4765 | St Etienne vs Brest | 2.26 | 3.21 | 3.21 |
| 18:00 | 4999 | SCR Altach vs LASK Linz | 4.88 | 3.71 | 1.60 |
| 18:00 | 5354 | Josko Ried vs WSG Wattens | 2.20 | 3.30 | 2.91 |
| 19:30 | 1085 | Monchengladbach vs FC Koln | 1.98 | 3.75 | 3.35 |
| 19:30 | 1283 | Juventus vs Bologna | 1.39 | 4.46 | 7.99 |
| 19:30 | 1395 | Valencia vs Osasuna | 2.13 | 3.22 | 3.58 |
| 19:45 | 5357 | Fortuna Sittard vs Sparta Rotterdam | 2.52 | 3.11 | 2.77 |
| 20:00 | 1483 | Maritimo vs Boavista | 2.45 | 3.08 | 2.93 |
| 20:00 | 3654 | Maccabi Haifa vs Bnei Sakhnin | 1.23 | 5.03 | 11.60 |
| 20:00 | 4525 | Zrinjski Mostar vs FC Sarajevo | 1.38 | 4.28 | 7.01 |
| 20:10 | 1598 | Lokomotiva Zagreb vs HNK Rijeka | 2.42 | 3.27 | 2.63 |
| 20:30 | 3647 | Fenerbahce vs Goeztepe | 1.37 | 4.79 | 7.39 |
| 20:30 | 4408 | Kaizer Chiefs vs SuperSport Utd | 2.10 | 2.92 | 3.82 |
| 21:00 | 5125 | Wisla Plock vs Lech Poznan | 5.28 | 3.91 | 1.53 |
| 21:45 | 4375 | Lazio vs Torino | 1.61 | 3.86 | 5.22 |
| 22:00 | 4457 | Lille vs Lens | 2.01 | 3.41 | 3.66 |
| 22:00 | 4535 | Getafe vs Villarreal | 3.04 | 3.09 | 2.46 |
| 22:00 | 4803 | Montreal Impact vs Vancouver Whitecaps | 1.75 | 3.78 | 4.44 |
| 22:30 | 1031 | Goias vs Palmeiras | 6.42 | 3.74 | 1.48 |
| 22:30 | 1168 | San Jose Earthquake vs Nashville SC | 2.84 | 3.34 | 2.45 |
| 22:30 | 3955 | Porto vs Portimonense | 1.14 | 7.37 | 16.94 |
| 23:00 | 4759 | Real Santander vs Deportes Quindio | 3.55 | 3.11 | 2.01 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# NYONI:TUMEJIPANGA KWA ORLANDO

**Na Dennis Fussi**

KIUNGO wa Simba, Erasto Nyoni amesema watapambana kwa nguvu zaidi, ili kuifunga Orlando Pirates na kutinga Nusu Fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu huu.

Mkongwe huyo amesema pamoja na kuanzia nyumbani, lakini wanapaswa kucheza kwa umakini na kutumia vizuri kila nafasi watakayoipata kwenye mchezo huo.

"Tunacheza na timu nzuri na ngumu, hatupaswi kujiamini hata kama tunacheza nyumbani," alisema Nyoni.

"Wenzetu wana uzoefu na mashindano haya, hivyo lazima tuwape heshima yao na kutimiza ipasavyo kila ambacho kocha atatuagiza," amesema.

Kiungo huyo amesema hawapaswi kuingia uwanjani na matokeo sababu mpira wa siku hizi una mabadiliko makubwa na timu nyingi zimejipanga, hivyo kila mchezaji atakayepata nafasi ya kuanza lazima acheze kupigania mafanikio hayo.

Nyoni amesema pamoja na yote, lakini anaamini timu yao safari hii wamejipanga vizuri na watashinda mchezo huo wa Jumapili dhidi ya Orlando Pirates na kutimiza malengo yao.

Kiungo huyo pia ameaomba mashabiki wao kujitokeza kwa wingi uwanjani, kuwaunga mkono, ili kuweka historia mpya ya kutinga nusu fainali kwenye michuao hiyo ya Afrika.



TIMU ya Taifa ya Wanawake Tanzania chini ya umri wa miaka 17, 'Serengeti Girls' wakiwa mazoezini kujiandaa na mchezo wao wa leo ugenini, kufuzu kombe la Dunia dhidi ya Burundi.

# Serengeti Girls kazi moja tu kwa Burundi leo

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Wanawake ya Wanawake Tanzania chini ya umri wa miaka 17, 'Serengeti Girls', inashuka dimbani leo, kutafuta ushindi mbele ya wenyeji Burundi, ukiwa ni mchezo wa kufuzu Kombe la Dunia.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Serengeti Girls, Bakari Shime alisema wamejiandaa vizuri kiufundi, mbinu na akili kwa lengo la kuhakikisha wanapata ushindi katika mchezo huo wa ugenini.

Alisema kila kitu kipo vizuri na anaamini mechi hiyo itakuwa ngumu, lakini wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanafanikiwa kupata matokeo mazuri ugenini.

"Tumejiandaa vya kutosha tunacheza ugenini, siku zote mechi hizo zinakuwa ngumu lakini wanahitaji kupambana kuhakikisha tunafikia malengo yetu ya kupata matokeo mazuri katika mchezo huu dhidi ya Burundi," alisema Shime.

Alisema wana waheshimu wapinzani wao Burundi na watacheza kwa tahadhari kubwa kwa kujilinda na kutafuta ushindi katika mchezo huo ambao wanahitaji kupata nafasi ya kufuzu kucheza kombe la Dunia.

Michuano ya kombe la Dunia la Wanawake kwa wachezaji chini ya umri wa miaka 17 itafanyikka Oktoba mwaka huu nchini India.

Michezo

Jumamosi Aprili 16, 2022

Nipashe



## Lukaku arejea Chelsea



Nyota wa Simba, Peter Banda (aliyeruka juu) akijifua na wachezaji wenzake kuelekea mchezo wa robo fainali ya kombe la Shirikisho Afrika, CAF, dhidi ya Orlando Pirates utakaopigwa keshokutwa uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA**

# Nabi aikunia kichwa Namungo

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi amewaangalia wapinzani wao, Namungo FC na kusema wanahitaji kujiweka fiti zaidi kuhakikisha wanafanikiwa kupata pointi tatu katika mchezo dhidi yao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema hakuna mechi iliyokuwa rahisi mbele yao hasa wanapokwenda kukutana na timu ambayo iliwasumbua katika mzunguko wa kwanza.

Alisema katika mechi ya kwanza walitoka sare ya 1-1 wakiwa ugenini, ana imani watakuwa wamebadilika kwa sababu wamefanya mabadiliko benchi la ufundi na kuwa na kiwango bora zaidi.

"Namungo FC ina wachezaji wazuri ukiangalia benchi la ufundi tofauti na mechi ya kwanza, tunatakiwa kujiandaa kuhakikisha tunafikia malengo yetu ya kupata pointi muhimu katika michezo iliyopo mbele yetu," alisema Nabi na aliongeza.

"Kazi kubwa kwa sasa kuendelea ni kujiimarisha zaidi kila nafasi ukiangalia katika mechi iliyopita kuna baadhi ya wachezaji akiwemo Saido Ntibanzokiza na Fiston Mayele kucheza wakiwa wagonjwa," alisema Nabi.

Alisema baada ya mapumziko ya siku chache timu imerejea kambini ameona nyota hao na baadhi ya majeruhi kurejea uwanjani na matumaini makubwa ya mechi ijayo kuwa na kikosi kipana.

Nabi alisema kazi kubwa anayoifanya kwa sasa anaendelea kuisuka safu ya ushambuliaji  kuwa imara na kurejea ilivyo awali kushinda kila mechi katika ligi hiyo.

Yanga inashuka dimbani Aprili 23, mwaka huu ikiwakaribisha Namungo FC katika mchezo wa Ligi Kuu mzunguko wa Pili utakaopigwa, Benjamini Mkapa jijini Dar es Salaam.

# MAKOCHA SIMBA, ORLANDO UMAFIA

## ●●●Pablo asema ilikuwa ni rahisi kwao kunasa taarifa na kuwapeleleza wapinzani wao kutokana na...

**Na Adam Fungamwangwo**

KUELEKEA kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika kati ya Simba dhidi ya Orlando Pirates ya Afrika Kusini, makocha wa pande mbili Pablo Franco na Fadlu Davis, wameonekana 'kufanyiana umafia' kila mmoja akidai kunasa taarifa na mipango ya mwenzake.

**Kocha Mkuu wa Simba, Franco amesema kuwa ilikuwa ni rahisi kwao kunasa taarifa na kuwapeleleza wapinzani wao kutokana na kuwa ni timu kubwa ambayo taarifa zao ziko wazi, lakini pia ana baadhi ya watu wa benchi la ufundi ambao wameshawahi kufanya kazi nchini humo, hivyo kuifahamu timu hiyo na Ligi ya Afrika Kusini kwa ujumla.**

"Itakuwa ni mechi ya kimbinu, nimewafundisha wachezaji wangu jinsi ya kuitumia VAR, wanatakiwa kuwa makini kutofanya makosa, lakini wanatakiwa kucheza mpaka mwisho wa tukio, bila kuhofu kuwa filimbi itapigwa au la. Nimewaambia wacheze mpaka wasikie filimbi, kwa sababu unaweza ukauacha mpira kumbe wala hujaotea. Ni kwamba VAR ndiyo itaamua, kwani unaweza kujiona labda umeotea, ukafunga bao, kumbe VAR itaonyesha hukuwa umeotea, au ukaacha, kumbe hukuwa umeotea, nimezungumza nao kuhusu hilo," alisema kocha Pablo na kuongeza.

"Nina kocha hapa wa makipa ameshawahi kuzifundisha timu za huko, kwa hiyo anaijua Orlando Pirates na ligi ya huko, nina mchezaji ambaye ameshacheza huko (Bernard Morrison), pia nina watu wanaokusanya taarifa, lakini ile ni timu kubwa ambayo wala hupati tabu sana kuifuatilia, kujua inatumia mfumo gani, wachezaji gani wa kuchungwa, kwa sababu inaweka sana taarifa zake kwenye mitandao ya kijamii, kwa hiyo ni rahisi kujua mbinu zake na nini tunatakiwa tufanye," alisema Pablo.

Taarifa za ndani za klabu hiyo zinasema kuwa kocha huyo alikabidhiwa na viongozi wa Simba video tatu za Orlando Pirates ambazo imecheza hivi karibuni kwa ajili ya kuzifanyia kazi, ambazo ni dhidi ya JS Saoura ya Algeria, Al Hittihad ya Libya ambazo ni za Kombe la Shirikisho na moja ya mechi ya Ligi Kuu Afrika Kusini ya hivi karibuni.

Kocha Msaidizi wa Orlando Pirates, Davis, akihojiwa na vyombo vya habari nchini humo, kabla ya kuanza safari alisema wanakwenda kucheza mechi ngumu dhidi ya timu inayotumia vema uwanja wake wa nyumbani, lakini imejipanga na wameifuatilia timu hiyo na kujua maeneo ambayo wana nguvu na mapungufu.

"Tunakwenda kukurana na timu nzuri. Timu inapocheza hatua hii ni lazima uipe heshima yake. Tunakwenda kucheza nyumbani kwao huku tukichukua tahadhari kubwa kwani wanapocheza kwao wanakuwa ni hatari zaidi. Simba wana washambuliaji wenye kasi, hatutakiwi kufanya makosa, hivyo tumeyafanyia kazi mapungufu yao, nguvu yao ilipo, kwani hatutakiwi kufanya makosa mengi hatarishi," alisema kocha huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >